AMBOLA

SEASON 06

PALE MASHUJAA
WANAPOLISALITI TAIFA LAO

MTUNZI: PATRICK.CK



HADITHI HII NI MALI YA MWANDISHI NA HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA KWA HIYO HAIRUHUSIWI KUCHAPISHA, AU KUITUMIA KWA NAMNA NYINGINE HADITHI HII BILA RUHUSA YA MWANDISHI.HATUA KALI ITACHUKULIWA KWA YEYOTE ATAKAYEKIUKA MASHARTI HAYA..

HADITHI HII NI YA KUBUNI HAINA MAHUSIANO NA TUKIO LOLOTE LA KWELI.

SIMULIZI NYINGINE ZA MTUNZI PATRICK.CK

SIMULIZI ZA MAPENZI

1.MISS TANZANIA
2.SERENA
3.BEFORE I DIE
4.BEYOND PAIN

SIMULIZI ZA UPELELEZI

5.PENIELA
6.QUEEN MONICA
7.THE FOOTBALL
8.I DIED TO SAVE PRESIDENT
9.KIAPO CHA JASUSI
10.KIKOSI CHA SIRI
11.SIRI
12.SCANDAL(KASHFA)
13.CAPTURE OR KILL MISSION
14.JAMII YA SIRI

MAWASILIANO
0764294499

© 2020 Masimulizi.Haki zote zimehifadhiwa

ILIPOISHIA SEHEMU ILIYOPITA

“Julius hebu tueleze kwa kina nini hasa kilichotokea? Perfect ameuliwa na nani? Aliuliza mjumbe moja ambaye alikuwa anafuatilia kikao kile kwa mtandao.

Julius Mukoke aliinamisha kichwa kwa sekunde kadhaa halafu akasema.

“I did. I killed him.”

Wajumbe wote walihisi baridi ya ghafla. Mara Charles

Ombe aliinuka na kumtazama Julius kwa hasira.

“Who are you? Nani amekupa mamlaka ya kutoa hukumu ya kifo? Aliuliza Charles kwa sauti kali. Sura za wajumbe wote zilionesha mshangao mkubwa.

“Relax everyone” alisema Julius.

“Nakuuliza wewe ni nani hata ukaanza kutoa hukumu ya kifo ndani ya mtandao huu? Aliuliza tena Charles Ombe.

“Naomba mnisikilize ndugu zangu. Naomba mnipe dakika chache mnisikilize” aliomba Julius. Bado minong’ono iliendelea hadi pale mmoja wa wajumbe aliyekuwa anafuatilia kwa mtandao alipoomba Julius apewe nafasi ya kueleza sababu za kumuua Perfect.

“Usiku huu, kupitia vyanzo vyangu nimepokea taarifa isiyo na shaka hata kidogo kuwa Bernadetha aliuawa na Joseph Tshibanga” alisema Julius na kuwaacha watu wote midomo wazi.

“Joseph? That’s impossible! Alisema Charles Ombe.

“Baada ya kumuua Bernadetha, Joseph Tshibanga naye aliuliwa na mtu anaitwa Thomas Ngalula. Nimeambiwa huyu ni mfanyakazi katika ubalozi wa Congo hapa Tanzania na ni mmoja wa watu walio katika mtandao wa Congo mpya. Simfahamu huyo Thomas ila tunaendelea kuchunguza na hadi kufika kesho atakuwa amepatikana.” Julius alinyamaza kidogo. Bado nyuso za wajumbe

zilikuwa na mshangao. Julius aliendelea.

“Huyo Thomas Ngalula kwa sasa anashirikiana na akina Mathew. Baada ya mauaji hayo kufanyika, Gosu Gosu alirejea kwa akina Mathew Mulumbi ambao wamepiga kambi yao hapa Dar es salaam mahali pa siri. Taarifa niliyoipata inasema kuwa usiku huu simu ya Perfect imeunganishwa kitaalamu na kompyuta ya akina Mathew hivyo kuwawezesha kufuatilia

mawasiliano yake yote ya simu.”

“What? Alisikika mmoja wa wajumbe.

“Hawa jamaa wanatumia teknolojia kubwa kwani kwa msaada wa Faraji Dilele wameweza kuingia katika mfumo wa SNSA bila sisi kufahamu na wanautumia mfumo huo kufanikisha mambo yao mbali mbali. Baada ya kupata taarifa hiyo nilifanya maamuzi ya kwanza kwa kumtaka Perfect azime simu yake na kutoa betri ili

kuwazuia akina Mathew kuendelea kufuatilia mawasiliano yake. Pili nilituma vijana wangu kwenda kumuua kabisa kwa sababu tayari ni mtu hatari kwetu. Tatu nilituma vijana wangu kumfuata Faraji Dilele ambaye alikuwa amejificha nyumbani kwa mwanaye Musa Faraji mfanyakazi wa SNSA. Taarifa niliyoipata ni kuwa Faraji na mwanaye wote wameuawa. Kwa sasa tayari kuna timu iko kazini kutafuta maficho ya akina Mathew Mulumbi.”alisema Julius.

“Dah ! sikujua kama mambo yako namna hii. Hawa watu kumbe wamepiga hatua kubwa namna hii. Hata hivyo bado sioni sababu ya kumuua Perfect. Kama simu yake tayari ilizimwa angetafuta simu nyingine. Hakuna sababu ya msingi iliyopeleka Perfect akauawa” alisema mmoja wa wajumbe.

“Kuna kitu kimoja ambacho hamkifahamu. Perfect alikuwa mtu hatari sana kwetu. Kuna yule msichana Ambola kutoka mtandao wa Congo ambaye

alikuwa akiishi nyumbani kwa Perfect, yule anatumiwa na akina Mathew. Perfect alikuwa na mahusiano ya kimapenzi na yule msichana bila kufahamu kuwa anatumiwa na maadui zetu. Kama tungemuacha hai Perfect basi tungekuwa katika hatari kubwa sana. Misheni nzima ingeharibika. Mnataka hilo litokee? Alihoji Julius. Chumba kilikuwa kimya. Baada ya muda mwenyekiti akasema.

“Maelezo hayo ya mwisho yametoa picha pana kabisa ya hatari iliyokuwepo mbele yetu

na sasa ninakuunga mkono kwa hatua uliyoichukua. Tumeumia sana kwa kifo cha mwenzetu lakini ulichokifanya ndicho kilichotakiwa kufanywa. Misheni hii lazima tuilinde kwa gharama zozote na kuhakikisha tunaifikisha mwisho. Pamoja na kukupongeza nataka kufahamu wapi alipo Ambola kwa sasa? Una mpango gani na Gavana?

"Tayari nimetuma timu kwenda kumchukua Ambola. Yule naye atatusaidia sana kufahamu mahali alipo

Mathew Mulumbi. Kuhusu Gavana, usiku wa leo atauawa kwa sababu hatutamuhitaji tena. Nina uhakika mkubwa usiku huu wa leo Mathew Mulumbi na kundi lake watapatikana. Hawajui kama tayari tumewazuguka na muda wowote kuanzia sasa tutafahamu mahali walipojificha" alisema Julius kikao kikaendelea.

ENDELEA.....

Marafiki wa Ambola ambao walifika msibani kumpa pole kufuatia msiba wa Bernadetha ambaye waliamini ni mama yake mzazi,walijiandaa kuondoka. Wakati akiagana nao,alitokea mama mmoja jirani yao.

“Ambola kuna wageni wako” alisema yule mama ambaye alikuwa ameongozana na watu wawili,mwanamke na mwanaume aliyevaa suti ya bluu. Marafiki zake Ambola walimuaga wakaondoka ili

kumpa nafasi ya kuzungumza na wageni wake waliowasili.

“Habari zenu. Karibuni” alisema Ambola.

“Tunashukuru. Pole sana kwa msiba”

“Ahsante nashukuru”

“Samahani kwa usumbufu Ambola. Ninaitwa Dionizi Mkiwa,mwenzangu ni Saada Seif. Tunafanya kazi katika kampuni inayojishughulisha na utengenezaji wa majeneza. Tulipigiwa simu asubuhi ya leo na baba yako akatuomba tufike

jioni hii tuzungumze. Tukiwa njiani kuja hapa kuonana naye alitujulisha kuwa ametoka kidogo lakini akatuelekeza tuje kuonana nawe. Tunataka kukuonesha aina ya majeneza tuliyo nayo ili uchague jeneza la aina gani utapenda litumike katika mazishi ya mama yako" alisema Dionizi. Alionekana kijana mpole lakini mwenye kujiamini sana.

"Ahsanteni sana kwa kuja. Ziko wapi picha za majeneza niziangalie? Aliuliza Ambola.

“Tumeziacha katika gari. Kama hatutakusumbua ninaomba tuongozane ukazitazame ili ufanye uchaguzi.” Alisema Dionizi. Ambola alimgeukia Jack aliyekuwa karibu yake.

“Jack ninakwenda kuchagua jeneza” alisema Ambola na kuongozana na wale watu kuelekea katika gari lao.

Dakika moja baada ya Ambola kuondoka kuelekea nje, Jackline alipigiwa simu na Ruby ambaye alimtaka

amuokoe Ambola haraka sana kwani watu wale hawana malengo mazuri naye.

Mara baada ya kupewa maelekezo hayo, Jack alivua gauni jeusi alilokuwa amelivaa akalitupa chini. Ndani alikuwa na suruali ya Jeans na fulana. Alitoka mbio kuelekea nje kwenye maegesho ya magari. Watu walibaki wakimshangaa namna alivyokuwa anakimbia. Hawakuelewa nini kimetokea.

“Ambola !!! aliita Jack baada ya kumuona Ambola akiwa na wale jamaa nje ya

gari aina ya Noah yenye rangi nyeusi. Ambola aligeuka akamtazama Jack akikimbia kueleka mahali alipo.

“Jac……” Ambola alitaka kuita lakini ghafla alisukumwa akaangukia ndani ya gari ambako alidakwa na mtu mwingine aliyekuwamo garini.

Watu waliokuwepo msibani walibaki wakishangaa Jack akikimbia huku mkononi akiwa na bastola. Hawakuelewa kitu gani kilichokuiwa kinaendelea. Ni

Jack pekee aliyeelewa maana ya kitendo kile cha Ambola kusukumwa ndani ya gari. Alikuwa ametekwa.

Wakati watu wakiendelea kushangaa kile kilichotokea, ghafla Dionizi alichomoa bastola baada ya kumuona Jack akikimbia akiwa ameishika bastola mkononi. Alisita kuachia risasi kuelekea upande alipo Jack kwa hofu ya kuleta madhara kwa watu wengine. Aliachia risasi mbili hewani. Bastola yake haikuwa na kiwambo cha kuzuia sauti hivyo mlio ule wa risasi ulizua

taharuki kubwa sana pale msibani. Watu walikimbia wengine wakilala chini kuokoa maisha yao kwani hawakujua risasi zile zilimlenga nani.

Pamoja na taharuki kubwa iliyotokea baada ya risasi kupigwa hewani, Jackline Mo aliisikia sauti ya Ruby masikioni mwake ikisema “Save Ambola”. Baada ya kupiga risasi zile mbili hewani, Dionizi aligeuka na kumtazama Jack ambaye risasi zile hazikumpa hofu yoyote. Katika akili yake alikuwa na lengo moja tu la kumuokoa

Ambola. Dionizi aligeuza shingo yake akamuona Jack bado akiwafuata,alikuwa amewakaribia sana. Alinyoosha mkono wake kwa lengo la kumpiga risasi lakini Jack tayari alikwisha ng'amua kile ambacho Dionizi alitaka kukifanya. Mkono wake wa kulia uliokuwa umeshika bastola ulikuwa mwepesi sana. Kabla Dionizi hajaizinga bastola yake, alipigwa risasi ya bega katika mkono ule aliokuwa ameshika bastola. Risasi mbili nyingine zilimpata katika paja la mguu wa

kulia,akaanguka chini. Baada ya kuanguka chini,gari lile alimoingizwa Ambola, liliondoka kwa kasi kubwa na kumuacha Dionizi akigaa gaa chini. Jack aliachia risasi kadhaa kuelekea katika lile gari lakini alichelewa,gari liliondoka kwa kasi kubwa.

Haraka haraka alimfuata Dionizi pale chini akalichana shati lake akamfunga mikono halafu akamuinua akamuweka begani akakimbia naye hadi katika gari lake. Alifungua mlango akamrushia ndani. Dionisi alikuwa anavuja damu.

Jack aliingia garini akaligeuza na kuondoka mahali pale kwa kasi akiacha taharuki kubwa imetanda pale msibani. Bado watu walikuwa wamepigwa na butwaa kwa kile kilichotokea. Lilikuwa ni tukio la muda mfupi ambalo lilionekana kama filamu fupi lililoacha gumzo.

Wakati watu wakiendelea kujiuliza kile kilichotokea,tayari Jack alikuwa amefika barabara ya Serengeti. Hakuliona lile gari lililomtorosha Ambola.

“Watakuwa wameeleka upande upi? Alijiuliza kwa sekunde kadhaa akiwa hajui aelekee upande upi. Mwishowe aliamua kuelekea upande wa kulia. Mwili ulikuwa unamtetemeka kwa hasira baada ya kushindwa kumuokoa Ambola.

“Nisaidie ! Nisaidie ! alilalama Dionizi ambaye alikuwa na maumivu makali huku damu ikiendelea kumvuja.

Jack alichukua simu yake akampigia Ruby.

“Jack” alisema Ruby baada ya kupokea simu. Jack alivuta pumzi ndefu.

“Jack are you okay? Aliuliza Ruby. Jack alishindwa ajibu nini.

“Jack ! aliita tena Ruby.

“Ruby” alisema Jack.

“Jack kuna nini? Hebu tulia na unieleze kile kilichotokea? Ambola yuko wapi? Aliuliza Ruby naye akianza kuingiwa na wasi wasi.

“Nimempoteza Ambola. Wamemchukua” alisema Jack

na kimya kikatawala. Ruby alivuta pumzi ndefu. Baada ya sekunde kadhaa za ukimya,Ruby akauliza.

“Imekuaje hadi wakafanikiwa kumchukua Ambola?

Jack alimueleza kile kilichotokea na kumpelekea ashindwe kumuokoa Ambola. Jackline alijilaumu sana.

“Usijilaumu Jack. Mambo kama hayo ni ya kawaida kutokea. Pamoja na kumpoteza Ambola,lakini tunaye mtu wao ambaye

ninaamini atatusaidia sana katika kujua mahali alikopelekwa Ambola.” Alisema Ruby na kumuelekeza Jack mahali ambako watakutana. Hakutaka kumuelekeza moja kwa moja mahali walipo.

“Nisaidie ninakufa ! alilalama Dionizi. Jack hakumjali aliongeza mwendo wa gari kuelekea mahali alikoelekezwa na Ruby wakutane.

****

Baada ya kuzungumza na Jack simuni, Ruby alimuita Jombaa.

“Jombaa ninatoka kidogo,kuna sehemu ninakwenda nitarejea baada ya muda mfupi. Naomba tafadhali mchunge sana huyu mwanamke.”

“Usiwe na hofu hata chembe.” alijibu Jombaa.

“Ahsante” alijibu Ruby na kutoka akikimbia hadi katika gari lingine ambalo alilitumia

Gosu Gosu kumpeleka Regina pale kiwandani. Aliondoka kwa kasi kuelekea mahali alikomuelekeza Jack wakutane.

Baada ya Ruby kuondoka,Jombaa huku akichechemea aliufungua mlango wa chumba alimo Regina.

“Jombaa ! Jombaa !aliita Regina.

Jombaa alimtazama halafu akatabasamu.

“Yule mwanamke ameondoka? Aliuliza Regina.

“Inakuhusu nini hata akiondoka? Aliuliza Jombaa.

“Kuna kitu nataka nikwambie.”

“Nini unataka kuniambia? Aliuliza Jombaa.

“Tumetoka wote Arusha, unakumbuka?

“Ndiyo ninakumbuka”

“Tafadhali naomba unisaidie. Hawa jamaa watakaporejea wataniua. Naomba unisaidie niweze

kuondoka mahali hapa. Nina pesa nyingi katika akaunti yangu ninataka nikusaidie na wewe pia. Nitakupa pesa nyingi na kukusaidia kuondoka hapa nchini kama utanifungua." Alisema Regina. Jombaa alitoa tena lile tabasamu lake la kinafiki na kuuliza.

"Utanipa kiasi gani cha pesa kama nitakusaidia kutoka mahali hapa?

"Kiasi chochote unachokihitaji nitakupatia.

Sema unahitaji kiasi gani? aliuliza Regina.

“Niambie ni kiasi gani utanipatia? Nikikwambia unipe milioni mia mbili utakuwa tayari kuzitoa?

“Nina pesa nyingi sana. Hata kiasi hicho unachokisema nitakupatia. Ninachohitaji mimi ni kutoka tu mahali hapa. Naomba unisaidie tafadhali”alisema Regina.

“Ulisema unaweza kunisaidia kwenda nje ya nchi. Ni vipi unaweza kulifanikisha hilo? Aliuliza Jombaa.

“Nina watu wanaoweza kunisaidia. Ni watu wazito. Tukitoka hapa tutakwenda kuonana nao na watatusaidia kuondoka hapa nchini” alisema Regina. Jombaa hakumjibu kitu alibaki akimtazama.

“Jombaa tafadhali naomba unisaidie. Hawa jamaa si watu wazuri hata kidogo hasa yule Mathew. Ni mtu mbaya sana.”

“Kimya ! alifoka Jombaa. Regina alishituka sana baada ya kuiona sura ya Jombaa ilivyobadilika ghafla.

“Unadhani nitaingia katika mtego kama ulivyomfanyia Gosu Gosu? Mimi ni jiwe na huwezi kunipata kirahisi. Sikiliza we mwanamke. Ninakufahamu vizuri wewe ni mtu wa aina gani. Ninakuhakikishia mwisho wako umefika. Hawa watu ambao unawaita wabaya wanapambana kwa ajili ya taifa hili bila kulipwa hata senti moja. Wameyaweka maisha yao katika hatari kubwa sana wakipambana na ninyi watu wenye mipango miovu dhidi ya nchi yetu.”

“Jombaa please help me! Everything they told you about me, are all lies”

“Unavyonisemesha kiingereza unazidi kunichafua.Ninaona kama vile unanitukana. Mimi sifahamu hiyo lugha ya kikoloni na ninaomba usiitumie tena unapozungumza nami. Ninakushangaa sana we mwanamke na mtandao wako kwa mambo ambayo mnataka kuyafanya. Kwa nini mnataka kuiharibu nchi hii kwa kufanikisha mipango ya mabeberu? Hata kama

mtafaidisha matumbo yenu kwa pesa mtakazolipwa na hao mabwana zenu mabeberu lakini ukumbuke wataoteseka ni babu na bibi zako kijijini kwa kukosa madawa huduma bora za afya,pembejeo nk. Watakaoteseka ni wanawake wenzak…. .”

“Stupid ! alisema Regina.

“Umesemaje? Aliuliza Jombaa kwa hasira.

“Huna msaada wowote na utakufa masikini. Nimekupa nafasi ambayo ungeitumia kubadilisha maisha yako,

umeshindwa kuitumia. Ninakuhakikishia utakufa masikini. Ninakufahamu wewe ni jambazi mkubwa lakini leo unajifanya una uzalendo mkubwa na taifa hili" alifoka Regina.

"Ninakubali mimi ni jambazi,nimefanya uhalifu mwingi,nimetoa pia roho za watu na hata wewe nililipwa nikutoe roho. Unapaswa kuwashukuru sana akina Mathew kwani bila wao hivi sasa tayari ungekuwa umekwisha anza kuliwa na wadudu kaburini. Nataka

ufahamu japokuwa mimi ni mhalifu lakini sijawahi kufikiria hata siku moja kuuza nchi yangu kwa mabeberu. Siwezi kufanya hivyo kwa sababu nina nchi moja tu ya Tanzania. Sina sehemu nyingine ya kukimbilia kama nchi hii itavurugika. Siwezi kuungana nawe katika ushenzi huo mnaotaka kuufanya. Nitaungana na akina Mathew kuhakikisha mipango yenu yote haifanikiwi. Nitashiriki katika kuhakikisha wewe na mtandao wako mnaishia aidha

gerezani au kaburini.” Alisema Jombaa.

“Hujui unachokisema. Tutaona mwisho wenu. Nakuhakikishia wewe na hao mbwa wenzako hamtafika kokote! Itumie nafasi hii kutengeneza maisha yako badala ya kuwa mtumwa wa hawa wajinga” alisema Regina.

“Maneno yao ya kejeli na dharau hayatakusaidia chochote. Mbio zako za sakafuni hapa zimegota ukingoni. Hebu jiandae kisaikolojia we mwanamke

kwa sababu mwisho wako tayari umefika.” Alisema jombaa na kutoka akaufunga mlango.

“Mwanamke mshenzi sana yule alijaribu kutaka kunishawishi na mimi nikubaliane naye. Hapa amekutana na jiwe,sitikisiki. Ni mara ya kwanza ninaahidiwa fedha nikazikataa. Hii ni kwa sababu nimemuelewa vizuri Mathew Mulumbi na kushuhudia mambo ambayo yeye na wenzake wanayafanya kwa ajili ya nchi hii. Hivi sasa ni

usiku,watu wanajiandaa kulala bila kufahamu kuna wanaume wako kazini kuhakikisha wao wanalala usingizi mzuri na kuamka kesho wakiwa salama. Nimeipenda timu hii na ninataka kuungana nao. Yawezekana hii nafasi ambayo Mungu anataka kuitumia ili kunibadilisha na kuwa mtu mpya. Ninaamini hivyo kwa sababu tangu Mathew alivyonieleza yale maneno machache asubuhi nimejikuta nikiwaza sana kuhusu hatima ya maisha yangu.
Nilichokisikia si sauti ya

Mathew. Ni sauti ya Mungu ndiyo maana nimepata wivu mkubwa na nchi yangu." Aliwaza Jombaa na kukumbuka kitu.

"Nimewaza kuhusu Mungu lakini sikumbuki lini mara ya mwisho nimehudhuria nyumba ya ibada walau kumshukuru kwa uhai alionijaalia. Nadhani huu ni muda wangu wa mabadiliko. Nimekutanishwa na hawa watu ili niweze kubadilika. Ninayakubali mabadiliko hayo kwa moyo mmoja na kuanzia nitaungana na hawa jamaa

katika mapambano ya kuipigania nchi yangu.” aliwaza Jombaa.

****

Jacklini Mo, alifika mahali alikopanga kukutana na Ruby. Ni katika uwanja wa mpira wa shule ya sekondari Mwishala. Alizima gari akashuka huku bastola yake ikiwa mkononi tayari kukabiliana na hatari yoyote inayoweza kujitokeza.

“Ambola utanisamehe sana kwa kushindwa kukuokoa katika mikono ya wale jamaa. Mazingira yalikuwa magumu, hata hivyo ninaahidi kushirikiana na akina Mathew Mulumbi kuhakikishia unapatikana. Huyu mshenzi ambaye aliongoza zoezi la kukuteka ataonesha mahali ulipo.” Aliwaza na kuufungua mlango akawasha tochi ya simu akammulika Dionizi ambaye alikuwa amechafuka damu kila mahali.

“Nina wasi wasi huyu jamaa anaweza akapotea

maisha kabla hajasema chochote. Ni huyu pekee ambaye ninamtegemea aoneshe mahali alikopelekwa Ambola" aliwaza Jack na kutazama kila upande lakini hakukuwa na dalili za gari lolote linaloelekea upande ule.

"Wakati ninamsubiri Ruby ngoja nifanya jitihada za kuzuia damu kuendelea kuvuja." Aliwaza Jack na kuvua fulana yake aliyokuwa ameivaa akaichana na kuweka mgandamizo katika sehemu zenye majeraha ya risasi.

“Nisikilize vizuri we jamaa” alisema Jack.

“Naomba unisaidie dada yangu ninakufa” Dionizi aliendelea kulalama.

“Nisikilize ninachokwambia ama sivyo utakufa kweli. Utavuja damu hadi ufe” alisema Jack halafu akamtazama Dionizi ambaye kwa wakati ule alihitaji sana msaada wowote.

“Ninataka kukusaidia. Nitakufungua mikono, nataka uweke mgandamizo katika paja lako mahali

ulikojeruhiwa. Ukithubutu kufanya ujinga wowote nitakumaliza” alisema Jack na kumfungua Dionizi mikono akaweka mgandamizo mahali penye majeraha ili kuzuia damu kuendelea kuvuja.

Haraka haraka Jack aliichomoa bastola yake baada ya kuuona mwangaza wa gari. Alijificha na kujiweka tayari kukabiliana na hatari yoyote. Gari lile lilisimama mita chache kutoka gari la Jack. Zilipita sekunde chache mlango ukafunguliwa akashuka Ruby. Jack alishusha

pumzi baada ya kumuona Ruby. Alisimama na kuita.

“Ruby”

“Ruy alipiga hatua za haraka haraka na kitu cha kwanza kilichomshangaza ni kumkuta Jack akiwa na sidiria nyeusi.

“Nini kimetokea? Aliuliza Ruby. Jack alimweleza kila kitu kilichotokea. Ruby alivua fulana yake akampa Jack avae. Yeye alibakiwa na fulana ndogo iliyokatwa mikono aliyokuwa ameivaa ndani ya fulana.

“Mfunge mikono, hawa watu si wa kuwaamini hata kidogo” alisema Ruby. Jack alimfunga mikono Dionizi halafu akashushwa akaingizwa katika gari la Ruby.

“Choma moto hilo gari lako” alisema Ruby. Jack akashangaa.

“Hili ni gari la Ambola” alisema Jack.

“Hata lingekuwa la nani hatulihitaji kwa sasa. Lichome moto. Kuna uwezekano likawa na kifaa cha kulifuatilia mahali lilipo. Lichome moto tafadhali”

alisema Ruby na kufungua sehemu ya nyuma ya gari lake akatoa galoni lililokuwa na petrol akampatia Jack pamoja na kiberiti.

“Kumbe ulikwisha jiandaa kabisa” alisema Jack huku akilipokea lile galoni akafungua mlango akamwagia petrol ndani ya gari. Alisimama nje akalitazama gari lile. Alikuwa anajishauri kama alichome moto au vipi.

‘Jack hatuna muda wa kupotexza. Washa kiberini tondoke mahali hapa” alisema

Ruby. Jack alichukua mti akafunga kitambaa akakiwasha na kukirushia garini. Aliingia katika gari la Ruby lakini kabla hawajaondoka Ruby alimtaka Jack ampatie simu yake. Baada ya kupewa simu alishuka akaitupia katika moto halafu akarudi garini wakaondoka kwa kasi kubwa.

“Imeniumiza sana kuharibu gari zuri kama lile” alisema Jack.

“Jack jielekeze kwa huyo jamaa. Tunamuhitaji sana”

alisema Ruby wakati akiliondoa gari kwa kasi ya ajabu huku wakiliacha gari lile la Ambola likiteketea kwa moto. Baada ya kuondoka eneo lile,Ruby alichukua simu yake akaitafuta namba Fulani akapiga.

“Ruby” alisema jamaa aliyepokea simu upande wa pili.

“Dkt Philip. Samahani kwa usumbufu. Nimekupigia ninaomba msaada wako” alisema Ruby.

“Nini unahitaji usiku huu Ruby?

“Kuna mtu amepigwa risasi anazo taar…….” Ruby hakumaliza alichotaka kukisema Dkt Philip akamkatisha.

“Ruby mmeanza tena mambo yenu. Lini mtapumzika hizi kazi Ruby? Where is Mathew? Aliuliza Dkt Philip. Ni wazi hakupendezwa na kile alichokiomba Ruby.

“Dkt Philip hayo mengine huu si wakati wake. Ninachohitaji ni kujua kama

utatusaidia au vipi. Tafadhali Dkt Philip ni muhimu sana" alisema Ruby. Kilipita kimya cha sekunde kadhaa.

"Dakika ishirini zijazo ninatakiwa kuwepo ndani ya chumba cha upasuaji hospitali kuu ya Mtodora. Nimepigiwa simu wananiomba niende hapo kuna upasuaji mgumu wa mapacha walioungana. Hebu tafakari wewe mwenyewe je niache kuhudhuria upasuaji huo wa kuokoa maisha ya watoto hao,nije kumtoa mgonjwa wenu risasi?. Ungekuwa mahali pangu

ungefanyaje? Aliuliza Dkt Philip. Ruby alivuta pumzi ndefu.

“Dkt Philip kazi yako ni kuokoa uhai wa watu na kitendo cha kushindwa kushiriki katika upasuaji huo kitakuumiza sana lakini linapokuja suala la maslahi ya nchi, mambo mengine yote tunayaweka pembeni tunaitanguliza nchi kwanza. Madaktari wako wengi ambao watashiriki katika upasuaji huo. Kukosekana kwako hakutaathiri kitu chochote. Umenitaka nifanye

uchaguzi,mimi ninataka uachane na huo upasuaji ili umuhudumie mtu ambaye kama akifariki dunia tutakosa kufahamu mambo muhimu kwa usalama wa nchi hii" alisema Ruby.

"Mathew Mulumbi tayari amewaaribu. Nitazungumza naye. Hii itakuwa ni mara ya mwisho kufanya kazi zake. Find another doctor" alisema kwa ukali Dkt Philip.

"Ahsante Dkt Philip" alisema Ruby.

“Mgonjwa huyo yuko wapi? Aliuliza Dkt Philip.

“Katika kile kiwanda kipya cha kusindika maziwa.”

“Sawa nitafika hapo.”

“Kuwa makini Dkt Philip” alisema Ruby.

“Umesahau hata mimi nimewahi kupitia mafunzo ya ujasusi ndiyo maana Mathew hasiti kunionesha sehemu zake zote muhimu” alisema Dkt Philip na kukata simu.

****

Dionizi alishushwa akaingizwa katika moja ya ofisi zilizo ndani ya jengo la utawala. Alilazwa sofani wakati wakimsubiri Dkt Philip awasili.

“Ruby nina hofu. Sijui nitamueleza nini Mathew Mulumbi kwa kumpoteza Ambola.” Alisema Jack.

“Narudia tena Jack, usijilaumu kwa kile kilichotokea. Mambo kama haya yanatokea katika misheni. Ulijitahidi kufanya

kila ulichoweza lakini tulichelewa. Hata hivyo ni kwa umahiri wako mkubwa tumefanikiwa kumpata huyu jamaa. Nina uhakika kuna mengi tutayapata kutoka kwake,pia kutoka kwa Regina. Kama akina Mathew watafanikiwa kumpata mke wa Gavana itatusaidia sana kufahamu mambo mengi.”

“Sijakuelewa Ruby. Regina yupi unamzungumzia? Mke wa Gavana naye amefanya nini? Aliuliza Jack. Ruby alimweleza kila kitu kilichotokea hadi wakafahamu kuwa Regina

alikuwa na simu akiwasiliana na mke wa Gavana. Kupitia simu hiyo ya Regina ndipo waliweza kugundua kuwa Ambola alikuwa katika hatari kubwa.

“Dah ! sikutegemea kama mchezo ungebadilika namna hii. Regina alionekana kama Malaika kumbe ni shetani mkubwa ! alisema Jack.

“Hata sisi bado tunashangaa namna jambo hili linavyokwenda. Regina alitakiwa kuuawa na akina Bernadetha, akanusuriwa na

akina Mathew. Papo hapo kumbe ana mawasiliano na mke wa Gavana. Tuna uhakika mkubwa waliomteka Gavana ni mtandao huo huo wa akina Barnadetha baada ya kufahamu alikutana na Mathew usiku wa jana. Kitendo hicho cha Regina kushirikiana na mke wa Gavana ambaye naye anashirikiana na akina Barnadetha kinaleta maswali mengi na kulifanya jambo hili liwe gumu zaidi.” alisema Ruby.

“Ruby unadhani Mathew Mulumbi atanielewa kwa tukio hili la kumpoteza Ambola? Nina wasi wasi anaweza akahisi nimefanya makusudi kwa kuwa ninalipwa fedha na Perfect kumlinda Ambola. Anaweza akanitoa katika misheni hii” alisema Jack kwa wasi wasi.

“Mathew Mulumbi ni binadamu wa ajabu sana. Kuna wakati anafikiri na kufanya mambo ambayo wengine hatuyafikiri. Ni mimi ambaye nilikuwa na wasi wasi nawe lakini Mathew alinitoa

wasiwasi. Alikuamini mara tu alipokutia machoni hivyo usiwe na hofu yoyote. Tunahitaji nguvu zaidi katika misheni hii. Kama kweli umeamua kushirikiana nasi basi shirikiana nasi kwa moyo mmoja. Ikigundulika u ndumila kuwili au umetusaliti kwa namna yoyote ile nakuhakikishia hawa jamaa ni watu wabaya mno. Mathew anachukia usaliti. Sipati picha kile kitakachomkuta Regina" alisema Ruby.

"Ruby mimi siwezi kufanya hivyo hata kidogo.

Mimi ni mzalendo wa kweli. Ninaipenda nchi yangu. Niliikubali kazi ile ya kumlinda Ambola kwanza kwa kuwa maslahi yake ni manono vile vile sikufahamu kile kilichokuwa kinaendelea nyuma ya pazia. Ni ninyi mlionifumbua macho nikafahamu kila kitu. Niko tayari kuungana nanyi katika mapambano haya….”

“Mimi pia niko tayari” ilisema sauti ya Jombaa aliyetokea nyuma ya mahali walipokuwa wamekaa akina Ruby.

“Nimesikia mazungumzo yenu. Mimi pia niko tayari kujiunga nanyi” alisema Jombaa.

“Karibu sana Jombaa. Anaendeleaje yule mwanamke? Aliuliza Ruby na Jombaa akawaeleza namna Regina alivyojaribu kumshawishi amuachie huru.

“Ulifanya vizuri Jombaa.” Alisema Ruby.

“Ilikuaje Gosu Gosu akakubali kurubuniwa na huyu mwanamke?

“Forgive Gosu Gosu. Ni mdhaifu sana kwa wanawake.” Alinyamaza Ruby baada ya simu yake kuita. Alikuwa ni Dkt Philip ambaye alimjulisha kuwa tayari amefika mahali pale. Ruby alikwenda kumpokea. Alimsaidia kubeba mkoba wake wakaelekea katika chumba alimo Dionizi.

“Nimekubali kuja kwa sababu ya Mathew Mulumbi. Nimetoka naye mbali na ni yeye aliyenisaidia sana kuanzisha ile hospitali yangu. Nilikwama na kuona ndoto zangu za kuwa na hospitali

yangu mwenyewe zimeyeyuka ndipo alipojitokeza akanikwamua mahali nilipokwama na leo nina hospitali yangu. Ninamuheshimu sana Mathew kwa hilo lakini lazima afahamu kuwa hata mimi nina wagonjwa ambao wanahitaji huduma yangu. Hiki mlichokifanya leo sijakipenda hata kidogo” alisema Dkt Philip.

“Dkt Philip utatusamehe lakini hatuna mtu mwingine wa kumkimbilia zaidi yako. Mgonjwa huyu anazo taarifa

muhimu ambazo tunazihitaji na hatuwezi kumpeleka hospitali. Wewe mwenyewe unalifahamu hilo” alisema Ruby.

“Mathew yuko wapi?

“Ametoka atarejea baada ya muda kidogo” alisema Dkt Philip.

Maandalizi yalifanyika na Dionizi alianza kuhudumiwa.

****

Kikao kizito kilikuwa kinaendelea, pale simu ya Julius Mukoke ilipoita. Hakusumbuka kuitoa mfukoni kwani tayari sikioni aliweka kifaa cha kupokelea simu.

“Hallow” alisema Julius huku akiinuka na kutoka nje ya chumba cha mikutano.

“Boss, tumeimaliza ile kazi lakini kuna jambo limetokea.” Alisema mtu aliyempigia simu Julius.

“Nini kimetokea? Aliuliza Julius na kuelezwa kile kilichotokea msibani. Alishindwa kujizuia akajikuta akipiga ngumi ukuta kwa hasira.

“Wakati ninawatuma niliwapa angalizo muwe makini sana kuhakikisha mnamchukua Ambola kimya kimya. Sikuwaambia itumike risasi yoyote ile. ! alifoka Julius.

“Boss tulifuata maelekezo uliyotupa lakini wakati Ambola akikaribia gari letu alitokea

mtu akikimbia akiwa na bastola mkononi akamuita. Ambola alipomuona mtu yule alishituka na kumuita jina moja tu la Jack halafu akasukumwa kuingia katika gari. Kwa kuwa mtu yule alikuwa na bastola ilimlazimu Dionizi kupiga risasi juu ili kumzuia asisogee lakini mtu yule alifanikiwa kumpiga risasi akaanguka nje. Hatukuweza kumsaidia tukaondoka”

“Idiots ! alisema kwa ukali Julius. Alikuwa anahema haraka haraka.

“Mmelifanya jambo hili limekuwa kubwa na gumu sana. Dionizi lazima atakuwa katika matatizo makubwa. Na kama hao jamaa wakifanikiwa kumpata wakamuhoji basi watafahamu kila kitu. Kwa nini mmefanya ujinga wa namna hii? Aliuliza Julius huku akitoka katika jengo lile akaenda katika gari lake. Dereva alimfungulia mlango akaingia ndani.

“Tunakwenda wapi mkuu? Aliuliza dereva.

“*Safe house level 1*” alisema Julius na dereva akaondoka. Mara tu baada ya kuondoka alitafuta namba ya kamanda wa polisi kanda maalum ya Dar es salaam akampigia.

“Julius” alisema Apolinary Vincent kamanda wa polisi kanda maalum ya Dar es salaam.

“Kamanda Apolinary samahani kwa usumbufu”

“Bila samahani Julius”

“Kuna tukio limetokea usiku huu nyumbani kwa jaji mstaafu Perfect Lyimo. Umekwisha pata taarifa zake?

“Kuna matukio mawili yametokea usiku huu yanayohusiana na jaji Perfect. Kwanza ni tukio la kuuawa kwake yeye mwenyewe. Pili ni tukio la utekaji lililotokea nyumbani kwake ambako inadaiwa binti yake anaitwa Ambola ametekwa na watu wasiojulikana. Tukio lipi unalizungumzia kati ya hayo mawili?

“Ni hili la pili la kutekwa Ambola. Niliwatuma vijana wangu kwenda kumchukua Ambola kimya kimya lakini wakafanya ujinga mkubwa hadi wakalifanya tukio hilo kuwa kubwa.”

“Sikujua kama ni vijana wako waliofanya tukio hilo.”

“Katika tukio hilo kuna kijana wangu amejeruhiwa kwa risasi na hajulikani alipo. Naomba ufuatilie kujua kama kuna hospitali yoyote wamempokea mgonjwa aliyepigwa risasi.

TUnamuhitaji haraka sana huyo mtu.” alisema Julius.

“Taarifa niliyopewa na vijana wangu waliofika eneo la tukio muda mfupi baada ya tukio hilo kutokea,wanadai mtu aliyempiga risasi mtu wako ni mtu wa karibu na Ambola. Inadaiwa ni mwanadada ambaye tangu asubuhi alifika msibani akiwa na Ambola. Watu wanahisi labda ni mlinzi wake. Mwanadada huyo amefahamika kwa jina moja tu la Jack. Inasemekana baada ya tukio hilo kutokea,alimchukua

huyo jamaa aliyepigwa risasi akakimbia naye hadi katika gari lake na kuondoka naye. Tayari vijana wangu wako kazini hivi sasa kufuatilia namna tukio hilo lilivyotokea na kumfahamu huyo Jack ni nani na amempeleka wapi huyo mtu aliyemjeruhik wa risasi. Kama amempeleka hospitali tutajua. Nitakupa mrejesho pale tutakapopata chochote”

“Ahsante sana Kamanda. Tunahitaji sana kumpata huyo Jack na kufahamu mahali aliko

mtu wetu.” Alisema Julius na kukata simu.

“Ni nani huyo Jack? Amempeleka wapi Dionizi?. Aliwaza Dionizi.

“Kwa namna wanavyomuelezea anaonekana ni mtu hatari sana. Hata hivyo hawezi kutukimbia. Kokote aliko lazima atapatikana kabla ya mapambazuko. Mathew Mulumbi na kundi lake wamekosea sana kujaribu kucheza nasi. Ushujaa wake safari hii umempeleka kubaya sana. Mwisho wake umefika”

aliwaza Julius na kutolewa mawazoni na simu iliyoita.

“Jonas” alisema

“Boss nimekupigia kukujulisha kuwa tumelifanyia kazi lile suala la Thomas Ngalula”

“Good. Nini mmepata?

“Tumefanikiwa kupata taarifa kuwa Thomas Ngalula ni jasusi wa Congo hapa Tanzania. Anafanya kazi idara ya usalama katika ubalozi wa Congo hapa nchini Tanzania. Huyu ameingia katika

mtandao wa Congo mpya bila kufahamika kama ni jasusi na amekuwa akitoa taarifa ya mipango yote ya mtandao huo kwa serikali ya Congo. Kila kitu kinachopangwa na mtandao huo tayari serikali ya Congo wanakifahamu. Tayari tumefahamu mahali anakoishi hapa Dar es salaam. Tunahitaji maelekezo yako ili aidha tukamchukue au tummalize kabisa.” alisema Jonas.

“Jonas ahsante kwa kulifanyia kazi kwa haraka sana jambo hili. Yule ni mmoja wa watu hatari sana kwetu.

Anatakiwa apatikane usiku huu. Nataka timu ya watu watano waende kumchukua Thomas haraka sana. Jonas natoa angalizo,hakuna kufanya makosa.” alisema Julius.

“Nimekuelewa mkuu. Hakutakuwa na makosa yoyote” alisema Jonas na Julius akakata simu halafu akatikisa kichwa kwa masikitiko.

“Dah ! Sikutegemea kabisa kama misheni hii ya muda mrefu ingeingia kirusi katika hatua hizi za mwishoni. Bado

siku chache kampeni izinduliwe na kisha tutaingia kwenye uchaguzi. Baada ya hapo kitakachofuata ni kama kuishi peponi. Sisi na vizazi vyetu vyote tutaishi maisha ya raha kama malaika. Pesa tuliyoahidiwa ni nyingi mno ambayo hadi mjukuu wangu ataikuta. Siwezi kukubali akatokea mtu na kuvuruga mipango yetu. Nitahakikisha ninatumia kila mbinu kupambana na hawa virusi watu walioibuka na kutishia usalama wa misheni yetu kwa sababu mimi ndiye niliyepewa

jukumu la kuilinda misheni hii na kuhakikisha inakuwa salama” aliendelea kuwaza Julius.

Alifika *level 1 safe house* ambako Ambola alipelekwa baada ya kutekwa. Alishuka garini haraka haraka akaingia ndani. Jamaa watatu waliokuwa sebuleni walisimama haraka baada ya Julius kuingia. Alisimama akiwa na hasira mithili ya Nyati.

“Natamani nizamishe risasi katika vichwa vyenu

wajinga wakubwa ninyi! Mnawezaje kufanya jambo la kijinga kama mlilolifaya? Alifoka.

“Samahani boss” alisema mmoja wao.

“Kwa nini mkakubali kuondoka na kumuacha mwenzenu peke yake? Watu watatu mnamkimbia mwanamke mmoja? Kwa nini mlishindwa kupambana naye? Kwa uzembe wenu mlioufanya haijulikani hadi sasa wapi alipo Dionizi. Ninawaamini sana lakini kwa upuuzi

mlioufanya leo mmenisikitisha na sintawashirikisha katika misheni nyingine yoyote” aliendelea kufoka Julius. Wale jamaa hawakujibu walibaki wamesimama huku wameinamisha chini vichwa vyao.

“Yuko wapi Ambola? Aliuliza Julius.

“Yuko chumba no 4” alisema jamaa mmoja.

“Nipeleke haraka”

Julius aliongozana na yule jamaa kwenda katika chumba

alimo Ambola. Alipitisha kadi mlango ukafunguka Julius akaingia ndani.

“Hallow Ambola” alisema Julius huku akijilazimisha kutabasamu. Ndani ya chumba kile kulikuwa na sofa tatu na runinga. Kilikuwa ni kama chumba cha mapumziko.

“Ninaitwa Jacob Simndela. I work for your father” alisema Julius huku akimtazama Ambola kwa makini. Baada ya Ambola kusikia kuwa Julius anafanya kazi na baba yake ile

hofu aliyokuwa nayo ilianza kutoweka.

“Kwa nini niko hapa? Aliuliza Ambola.

“Samahani Ambola kwa usumbufu mkubwa ulioupata. Kuna mambo yametokea ambayo hukuwa umeyafahamu bado” alisema Julius.

“Mambo gani? aliuliza Ambola.

“Kuna jambo kubwa limetokea usiku huu,sina

hakika kama tayari umepata taarifa”

“Hapana bado sijapata taarifa. Nini kimetokea?

“Ni tukio linalomuhusu baba yako Perfect.”

“Nini kimemtokea baba? Aliuliza Ambola kwa wasi wasi.

Julius alivuta pumzi ndefu akatazama chini.

“Kuna nini Jacob? aliuliza Ambola.

“Baba yako amepigwa risasi”

Mshituko mkubwa ulionekana usoni kwa Ambola.

“Mungu wangu ! alisema huku akiipeleka mikono yake mahali ulipo moyo.

“Is he dead? Aliuliza Ambola.

“Amekimbizwa hospitali lakini hali yake si nzuri. Tuendelee kumuombea. Ambola nimekwambia jambo hili kwa kuwa naamini wewe ni jasiri. Hiki ni kipindi kigumu sana ambacho unatakiwa kuonesha ujasiri wako”

alisema Julius. Ambola akafuta machozi.

“Ambola huu si wakati wa kulia. Kama nilivyokwambia unapaswa kuwa jasiri sana kuliko wakati wowote. Umenielewa Ambola?

“Nimekuelewa. Nataka kufahamu,baba kapigwa risasi na nani? Aliuliza Ambola.

“Baada ya kupata taarifa za baba yako kupigwa risasi, tulianza kufuatilia mara moja na kugundua baada ya kumpiga risasi baba yako, watu hao walitaka kukufuata

na kukuua nawe pia ndipo nilipotuma watu haraka sana msibani ili waje wakuchukue kimya kimya. Hatukuhitaji kutengeneza tukio kwa sababu wale waliotumwa kukumaliza walikuwa tayari wamefika msibani. Hatukutaka kukueleza ili kuogopa kukushitua ndiyo maana wale jamaa nilio watuma walijifanya ni watu kutoka kampuni ya kutengeneza majeneza. Kwa bahati mbaya sana kuna mtu ambaye hakuelewa kilichokuwa kinaendelea, akahisi labda

watu wale wanataka kukuteka. Nimeambiwa kuna mwanamke mmoja alijitokeza akiwa na bastola hivyo kumlazimu mmoja wa vijana niliowatuma apige risasi juu ili kumzuia mwanamke huyo asiweze kuleta madhara yoyote. Hata hivyo bado mwanamke huyo alimpiga risasi mtu wangu hivyo kutengeneza tukio kubwa ambalo hatukutarajia litokee. Taarifa zinadai mtu huyo alimchukua mtu aliyepigwa risasi akaondoka naye kusikojulikana. Samahani sana Ambola kwa usumbufu

huu mkubwa uliotokea. Haikuwa lengo letu kukuletea usumbufu huu mkubwa hasa kwa wakati huu ambao unaendelea na maombolezo ya kifo cha mama yako” alisema Julius.

“Jacob ninahitaji kufahamu mambo mawili tu. Kama baba yangu amekufa naomba uniweke wazi. Jambo la pili nataka kujua nani waliomshambulia baba na wanataka kuniua na mimi?

“Ambola kuhusu baba yako bado hajafa japo hali yake

ni mbaya. Tayari amekimbizwa hospitali. Kwa taarifa nilizozipata tayari amekwisha anza kufanyiwa upasuaji. Tumuombee. Kuhusu nani kamshambulia hilo ninaliweka pembeni kwa sasa tunaendelea kuwafuatilia ni mtandao mrefu lakini tuna watu wetu ndani ya mtandao huo. Pale tutakapokuwa na taarifa za kutosha nitakujulisha. Kwa sasa tunataka kwanza kujiridhisha na hali ya kiusalama kabla ya kukupeleka hospitali ambako baba yako amepelekwa. Kuna kitu kimoja

ninataka unisaidie. Mwanamke yule ambaye amemchukua mtu wetu unamfahamu? Aliuliza Julius.

“Ndiyo ninamfahamu. Anaitwa Jacline Mo. Ni mlinzi na msaidizi wangu ambaye baba alinitafutia”

“Tunahitaji kuwasiliana naye ili kujua mahali alikompeleka yule mwenzetu ambaye tunataka kumtibu” alisema Julius kwa sauti ambayo ilimfanya Ambola amuamini.

“Namba yake iko katika simu yangu” alisema Ambola. Julius alitoka nje baada ya dakika chache akarejea ndani akiwa na simu ya Ambola. Alimpatia akaiwasha akaitafuta namba ya Jackline akampigia lakini simu yake haikupatikana.

“Simu yake haipatikani.” Alisema Ambola.

“Unadhani ni wapi anaweza akapatikana muda huu? Tuna wasi wasi asije akampeleka yule mtu hospitali. Atajiweka katiak matatizo

makubwa kwani jeshi la polisi linafanyia uchunguzi tukio lile. Tunahitaji kumsaidia haraka sana. Yeye katika mawazo yake anahisi labda wale watu walikuwa na malengo mabaya nawe. Kama kuna sehemu unahisi tunaweza kumpata tuelekeze tafadhali tutamuelewesha ili jambo hili limalizike kimya kimya na kumuepusha yeye pia kutoingia katika hatari. Akiingia katika hatari wewe pia utajikuta katika matatizo makubwa.” Alisema Julius.

Ambola alizama katika tafakari halafu akasema.

“Kuna sehemu moja tu ambako nahisi atakuwa amempeleka huyo mtu. Ni katika nyumba tunayoishi. Kwa siku za karibuni baba alinihamishia katika nyumba nyingine kwa muda kwa sababu za kiusalama” alisema Ambola.

“Nielekeze tafadhali mahali hapo ili tumfuate tumueleweshe na tulimalize suala hili” alisema Julius. Ambola alimuelekeza bila hofu

katika nyumba ile alikohamishiwa.

“Ahsante sana Ambola. Ninakwenda mahali hapo mimi mwenyewe ili kuona kama atakuwa hapo. Nikimpata nitakuja naye hapa kwa ajili ya usalama wake pia. Wakati huu ninakuomba uizime kabisa simu yako ili kuzuia wale wanaokutafuta kujua kama uko hapa” alisema Julius na kuichukua simu ya Ambola akatoka nayo nje. Alimchukua jamaa mmoja kutoka katika wale jamaa

watatu akaongozana naye kumfuata Jack.

“Nani kampiga Perfect risasi? Naanza kuhisi kuna mtafaruku katika mtandao wao ndiyo maana kumeanza kutokea mambo kama haya ya kupigana risasi. Ninamuombea mzee yule apone haraka.” Aliwaza na picha ya tukio lile lililotokea nyumbani ikamrudia kichwani. Sauti ya Jack akimuita bado ilipenya katika masikio yake.

“Nilimtaka Jack anisubiri ili nikazungumze na wale wageni lakini ghafla nilimuona akija akikimbia akaniita kama vile anataka kunipa onyo Fulani. Nadhani kama alivyosema Jacob, Jack alihisi labda nimetekwa ndiyo maana alitaka kuniokoa. Lakini bado kuna kitu sijakielewa. Jack nilimuomba anisubiri, alifahamuje kama wale watu ni watekaji? Kwa nini alikuja mbio namna ile? Nitakapoonana naye atanieleza kwa undani zaidi nini hasa kilichotokea. Kwa

sasa niendelee kumuombea mzee Perfect ili aweze kupona. Pamoja na mipango yao miovu kwa nchi lakini ana utu. Amenilea kwa upendo mkubwa tangu nilipotoka kambini akiamini mimi ni mkimbizi. Nilipata kila nilichokihitaji kutoka kwao. Ni hivi majuzi tu ndipo nilipoingia katika laana baada ya kuanza kutembea na yule mzee. Ni mtu mzuri. Naomba Mungu amsaidie ili apone" aliwaza Ambola.

****

Kwa kufuata maelekezo aliyopewa na Ambola, Julius alifika katika ile nyumba ambako Ambola alikuwa akiishi kwa muda. Mara tu waliposikia muungurumo wa gari, walinzi wawili wa kimasai walitoka.

“Habari rafiki” alisema Julius baada ya kushuka garini.

“Tukusaidie nini rafiki?

“Nimemfuata Jack yule msaidizi wa Ambola”

“Kuna wanawake wawili wanaishi humu ndani hatuwajui majina yao,mmoja mwembamba na mwingine mnene. Yupi unayemuhitaji?

“Yule mnene.” Alijibu Julius japo hakuwahi kumuona Jack ila alifahamu Jack ni mnene kwa kuwa Ambola hakuwa mnene.

“Wale wanawake hawajarudi hapa tangu walivyoondoka asubuhi.”

“Nimewasiliana naye muda si mrefu akaniambia anakuja hapa.”

“Hapana bado hajafika” alisema mmoja wa wale walinzi. Julius aliingia garini akafungua mkoba wake akatoa bunda la noti akawapatia wale walinzi.

“Hizo za kwenu. Mara tu atakaporejea naomba mnijulishe kwa kupitia namba hii” alisema Julius huku akiwapa namba yake ya simu.

“Msimweleze chochote kama nimekuja hapa kumtafuta” alisema Julius na kurejea garini akiwaacha wale walinzi wakishangaa baada ya

kupewa bunda lile la noti. Gari liligeuzwa na kuondoka. Julius alimpigia mmoja wa wale jamaa waliobaki nyumbani akamtaka ampelekee simu Ambola ili wazungumze.

“Hallo Jacob” alisema ambola.

“Ambola, nimefika hapa nyumbani nimewakuta walinzi wawili wa kimasai wamesema Jack hajafika hapa. Unahisi kuna sehemu nyingine anaweza kwenda?.

“Kama umemkosa hapo nyumbani, sifahamu mahali

pengine ambako atakuwa amekwenda.” Alisema Ambola.

“Ambola jaribu kufikiria. Lazima kuna sehemu amekwenda. Ninarejea hapo ili kufanya mpango wa kukupeleka hospitali ukamuone baba yako” alisema Julius na kukata simu.

“Kama Jackline hajarudi nyumbani sehemu pekee ambako atakuwa amekwenda ni kwa akina Mathew Mulumbi. Anaamini watu wale walitaka kuniteka. Kama

amekwenda kwa akina Mathew hili tayari ni suala lingine. Nao pia wataweka pembeni shughuli zao na kuanza kunisaka mimi. Natakiwa kuwasiliana na Ruby nimjulishe kile kilichotokea na kama Jack amekwenda kwao basi amuachie yule mtu aliyempiga risasi ili atibiwe. Atakaporejea Jacob nitamtaka anipe simu yangu niwasiliane na Ruby ili nifahamu kama Jack amekwenda kwao" aliwaza Ruby.

****

Julius alirejea safe house na moja kwa moja alikwenda katika chumba alimo Ambola.

“Ambola ninashukuru nimefika mahali uliponielekeza lakini sijamkuta Jackline ila nimezungumza na walinzi wameniahidi atakaporejea watanijulisha mara moja. Ni muhimu sana kumpata Jack usiku huu kabla hajampeleka hospitali yule mtu aliyempiga risasi. Kama akimpeleka hospitali atatuingiza sisi sote katika

matatizo. Suala hili tayari limefika kwa jeshi la polisi hivyo hatupaswi kufanya mzaha hata kidogo” alisema Julius.

“Jacob naomba simu yangu. Kuna mahali ninahisi Jack atakuwa amekwenda kama hajafika nyumbani.” Alisema Ambola.

“Ni wapi huko? Nielekeze tafadhali”

“Ni kwa rafiki yangu ambaye ni muuguzi. Nilimtuma jana akanichukulie dawa Fulani nadhani atakuwa

amekwenda kwake kuomba msaada. Naomba simu nizungumze naye ili nijue kama amefika kwake au vipi" alisema Ambola.

"Ahsante sana Ambola" alisema Julius akatoka baada ya muda mfupi akarejea akiwa na simu akampatia Ambola. Aliiwasha halafu akaitafuta namba ya simu ya Ruby akampigia.

"Ambola ! alisema Ruby huku sauti yake ikionesha alipatwa na mshangao mkubwa.

“Ruby habari yako”

“Dah ! Ahsante Mungu. Ambola uko wapi? Are you safe? Aliuliza Ruby

“Niko salama Ruby usihofu. Jack amefika kwako?

“Jack? Ruby alishituka kidogo.

“Ndiyo. Amefika kwako?

“Ndiyo Jack yuko hapa pamoja na mmoja wa wale watu waliotaka kukuteka”

“Ruby sikiliza. Wale watu hawakutaka kuniteka. Wale watu walitumwa kuja

kuniokoa. Kuna mambo yametokea usiku huu. Baba amepigwa risasi yuko hospitali sasa hivi”

“Amepigwa risasi?

“Ndiyo. Amekimbizwa hospitali”

“Nani kafanya tukio hilo?

“Haijulikani hadi sasa nani kafanya tukio hilo. Watu waliompiga baba risasi walikuwa na malengo ya kunimaliza na mimi pia,wakatuma watu wao kuja msibani kunimaliza lakini kwa

bahati nzuri kuna watu ambao wana ukaribu na baba waligundua hilo na wakafika pale msibani kwa lengo la kuninusuru. Walitaka kunichukua kimya kimya bila mtu yeyote kufahamu na hapo ndipo ilipoibuka sintofahamu kwani Jack aliamini watu wale wameniteka yakaibuka majibizano ya risasi nikaondolewa haraka mahali pale. Hivi sasa niko sehemu salama kabisa. Ninataka kufahamu kama Jack amekupigia simu au amefika kwako.” Alisema Ambola.

Ruby alivupa pumzi ndefu akasema.

“Ambola naomba unisikilize kwa makini sana na ninaomba kama uko na hao watu karibu usioneshe mshituko wowote kwa kile nitakachokwambia” alisema Ruby na kunyamaza kidogo.

“Inawezekana hao watu kuna maneno wamekwambia ambayo si kweli. Watu hao wametumwa kuja kukuteka. Watu hao ni mtandao ule wa akina Bernadetha na tayari wamefahamu kuwa

unashirikiana nasi. Tumeinasa simu ya Regina akiwasiliana na mke wa Gavana akamjulisha mambo mengi kuhusu sisi pamoja na misheni yetu. Hata tulivyoiunganisha simu ya jaji Perfect ili tufuatilie mawasiliano yake tayari wamefahamu kupitia Regina. Baada ya kugundua uko katika hatari kubwa, nilimpigia simu Jack nikamweleza kuwa uko katika hatari akaniambia kuna watu wamekuja kukuchukua nikamwambia afanye kila linalowezekana akuokoe lakini kwa bahati mbaya

hakufanikiwa. Ambola hao watu wanamtafuta Jack pamoja na yule mtu wao ndiyo maana wamekudanganya kuwa wamekuja kukuokoa. Wana hofu endapo tutamuhoji mtu wao basi tutapata mengi kutoka kwake.
Ninachokuomba jitahidi kupoteza wakati ili tufike mahali hapo kukuokoa. Nitafuatilia kujua simu hii imepigwa kutoka wapi halafu tutakuja kukuokoa. Tafadhali naomba uniamini Ambola uko katika hatari kubwa. Hao jamaa wakifanikiwa kukupata

wewe na Jack watawaua. Umenielewa Ambola? Aliuliza Ruby.

“Ahsante sana Ruby kwa msaada uliompatia Jack. Nitawasiliana na walinzi wangu kujua kama tayari amefika nyumbani. Ahsante sana” alisema Ambola na kukata simu halafu akamtazama Julius huku akilazimisha tabasamu.

“Huyu niliyezungumza naye ni rafiki yangu sana ambaye ni muuguzi. Kama nilivyohisi ni kweli Jack

alikwenda kwake akiwa na mtu aliyejeruhiwa kwa risasi kuomba msaada. Amemsaidia kumpa huduma mtu huyo kuzuia damu kuvuja lakini yeye hana uwezo wa kumtoa risasi. Amemtaka aende nyumbani wakati yeye anajitahidi kutafuta daktari ili ampeleke nyumbani akamuhudumie yule mtu. Hivi sasa tayari Jack amekwisha ondoka kwa huyo mtu na ameelekea nyumbani." Alidanganya Ruby.

"Ahsante sana Ruby. Hiyo ni habari njema sana.

Ninakwenda tena kule nyumbani kwako kumfuatilia Jack na kumleta hapa.” Alisema Julius huku akigeuka haraka na kupiga hatua kuelekea mlangoni. Kwa haraka aliyokuwa nayo alisahau kuichukua simu kutoka kwa Ambola. Alitoka mbio hadi katika gari lake akaingia na kuondoka kwa kasi kubwa kuelekea nyumbani kwa Ambola. Zilipita dakika chache,Ambola alichukua simu yake akampigia Ruby.

“Ambola” alisema Ruby

“Ruby tafadhali niambie yale uliyonieleza ni mambo ya kweli”

“Ni kweli Ambola. Hao watu ni mtandao wa akina Bernadetha na tayari wamekwisha fahamu unashirikiana nasi. Wanachokitafuta kwa sasa ni kumpata mtu wao.”

“Nimewadanganya kuwa Jack ameelekea nyumbani na wamemfuata huko. Ruby tafadhali naomba mfanye kila linalowezekana mnitoe mahali hapa” alisema Ambola huku

machozi yakimtoka baada ya kujaribu kufungua mlango na kukuta umefungwa.

“Ambola usikate hiyo simu. Tunaifuatilia kufahamu mahali ulipo. Ambola kuwa jasiri tunakufuata” alisema Ruby.

“Mwili wote unatetemeka kwa mambo aliyoniambia Ambola. Hawa watu kama kweli wamenifahamu basi niko katika hatari kubwa. Ni vipi kuhusu mzee Perfect ni kweli amepigwa risasi? Alijiuliza

Ambola huku machozi yakiendelea kumtiririka.

****

“Jack, tunatakiwa kwenda kumuokoa Ambola. Mathew wala Gosu Gosu hawapo hili ni jukumu letu sisi wawili kuhakikisha Ambola anakombolewa” alisema Ruby.

“Ruby niachie mimi kazi hiyo. Nielekeze mahali alipo niende tafadhali. Ni mimi niliyesababisha hadi Ambola

akachukuliwa. Naomba nipe nafasi hii nirekebishe makosa yangu” alisema Jack.

“Jack huwezi kwenda huko peke yako. Tunakwenda sote.” Alisema Ruby.

“Tukiondoka sote nani atabaki mahali hapa kuhakikisha kila kitu kinakwenda vizuri?

“Jombaa yupo atahakikisha kila kitu kinakwenda vizuri.” Alisema Ruby na kumfuata Jombaa katika chumba cha upasuaji alikokuwa anamsaidia Dkt

Philip akamtaka ampatie bastola yake ambayo ilifungwa kiwambo cha sauti.

“Jombaa kuna sehemu mimi na Jack tunakwenda,hakikisha kila kitu kinakuwa salama mahali hapa. Hatutachukua muda mrefu” alisema Ruby kisha kwa haraka aliongozana na Jack wakaingia garini wakaondoka kuelelekea mahali alikokuwa Ambola. Jack ndiye aliyeshika usukani wa gari lile huku Ruby akiwa makini katika kompyuta yake kuifuatilia ile simu ya Ambola

ili kujua mahali alipo. Bado simu ya Ambola ilikuwa hewani ili kumuwezesha Ruby kufahamu mahali alipo.

****

Julius alifika katika tena katika ile nyumba ya akina Ambola. Alishuika garini haraka akawafuata walinzi.

“Rafiki umerejea tena. Bado mtu wako hajarejea” alisema mmoja wa walinzi wale wa kimasai.

“Rafiki tafadhali naomba msinidanganye. Amenipigia simu akaniambia tayari amefika hapa. Naomba niingie ndani nikajiridhishe mimi mwenyewe kama kweli hajafika” alisema Julius.

“Hatuwezi kukuruhusu ukaingia ndani wakati wenyewe hawapo. Kama amekupigia simu basi msubiri atakuwa njiani anarudi” alisema mlinzi. Julius hakuwa na muda wa kupoteza. Alichomoa bastola yake.

“Mtaniruhusu niingie ndani au nitumie nguvu?

Walinzi wale walitetemeka baada ya kumuona Julius akiwa na bsatola. Walimfungulia geti ili aingie ndani, akawataka wote waingie ndani. Mlango wa sebuleni ulikuwa umefungwa,Julius aliurukia teke ukafunguka wakaingia ndani. Walikagua chumba kimoja baada ya kingine lakini hawakukuta mtu yeyote. Julius alichanganyikiwa.

“Ngoja niendelee kusubiri yawezana amekwama njiani na muda si mrefu atafika” aliwaza Julius akaenda nje kumsubiri Jack.

Akiwa nje ya gari lake alipigiwa simu na watu wake akajulishwa kuwa Thomas Ngalula tayari amepatikana. Alielekeza apelekwe *Level 1 safe house*.

“Hawa Panya wote ninaamini kabla ya mapambazuko leo watakuwa wamepatika. Tayari tunaye Gavana,Ambola,Thomas

Ngalula na muda si mrefu ninaamini atapatikana Jack na tutamkomboa mtu wetu.” Mara alikumbuka kitu. Akachukua simu yake akaitafuta namba ya Red akampigia.

“Boss” alisema Red.

“Red nini kinaendelea hadi sasa?

“Boss,bado tunamsubiri Mathew Mulumbi. Mpaka sasa hajatokea mahali alikopanga kukutana na Gavana.”

“Red,kama hatatokea baada ya nusu saa,mrudishe nyumbani mara moja halafu tutajua nini cha kufanya” alisema Julius na kukata simu.

“Viongozi walinitaka nimuue Gavana lakini suala hilo bado sikubaliani nalo hata kidogo. Kama akiuawa, tutamtibua Lucy mke wake. Hatukukualiana Gavana aumizwe au auawe. Vile vile yule mzee kuna mambo mengi anayafahamu hivyo bado tunamuhitaji sana” aliwaza Julius. Bado aliendelea kumsubiri Jack afike.

****

Programu aliyoitumia Ruby kufuatilia simu ya Ambola,iliwasaidia kufika mahali alipo.

“Programu inanionesha ni katika nyumba ile pale ndimo alimo Ambola.” Alisema Ruby.

“Hakuna mlinzi yeyote nje lakini taa zinawaka ndani kuashiria kuna watu” alisema Jack.

“Sikiliza Jack, hawa watu hawatufahamu sisi ni akina

nani. Vile vile hawategemei kama tunaweza kufahamu kama Ambola yuko mahali hapa. Tunachofanya tunakwenda na gari hadi getini,tutapiga honi na kuwafanya watoke kuja kuangalia ni nani amekuja. Kuna mawili yanaweza kutokea. Moja wanaamini kuwa gari lolote litakalofika mahali hapa lazima lina mahusiano na wao hivyo wanaweza wakahisi sisi ni wenzao. Pili wanaweza wakagundua kuwa sisi hatuna mahusiano nao hivyo

yakaibuka mapambano. Vyovyote vile itakavyokuwa lazima tuhakikishe tunampata Ambola” alisema Ruby.

“Nimekuelewa Ruby.”

“Good. Twende kazini” alisema Ruby. Jack alilielekeza gari katika geti la ile nyumba. Taa isiyo na mwangaza mkali ilikuwa inawaka getini. Jack alipiga honi mara mbili wakasubiri. Bastola ya Jack ilikuwa katika mkono wake wa kulia tayari kabisa kukabiliana na chochote kitakachotokea.

Jack alipiga tena honi baada ya kupita dakika moja bila geti kufunguliwa na safari hii mlango mdogo wa geti ulifunguliwa. Jamaa mmoja aliwasogelea kutaka kufahamu ni akina nani.

“Take him” alielekeza Ruby. Jack aliiweka sawa bastola yake. Jamaa alipofika usawa wa dirisha,Jack alishusha kioo cha dirisha na kwa kasi ya aina yake aliachia risasi mbili zilizompeleka jamaa ahera. Yalikuwa ni mauaji ya kimya kimya kwa kuwa bastola aliyoitumia Jack

ilifungwa kiwambo cha kuzuia sauti. Haraka haraka walimvuta yule jamaa na kumuingiza katika gari lao.

“Twende tukamtafute Ambola.” alisema Ruby. Kwa kutumia ule mlango mdogo pembeni ya geti waliingia ndani. Kulikuwa kimya kabisa. Kwa tahadhari walifika katika mlango wa kuingilia sebuleni. Ruby alimpa ishara Jack ajiweke sawa,akakinyonga kitasa cha mlango akaufungua.Kwa kasi ya aina yake Jack akarukia ndani. Pale sebuleni walimkuta

mwanadada mmoja akiwa ametulia akitazama runinga. Mwanadada yule macho yalimtoka pima baada ya kujikuta akitazama na bastola ya Jack.

“Usijaribu kupiga kelele nitakufumua kichwa chako kwa risasi! Alionya Jack. Ruby alishika kitanza mbali akaongeza sauti ya runinga halafu akamsogelea yule mwanamke.

“Wenzako wako wapi? Aliuliza. Mwanamke yule alisita kujibu. Mezani kulikuwa

na bastola,kisu na mabaki ya matunda. Kwa kasi ya umeme Ruby alinyoosha mkono wake akakichukua kile kisu akakizamisha katika paja la yule mwanamke.

“Aaaagghh ! alipiga ukelele. Jack aliyekuwa karibu alimrukia teke akaanguka sofani Ruby akamziba mdomo,akamuelekezea kisu machoni.

“Nitakutoboa jicho moja baada ya lingine. Wenzako wako wapi? Aliuliza Ruby.

“Hawapo. Tuko wawili tu” alijibu.

“Ambola yuko chumba gani? aliuliza Ruby.

“Simfahamu Ambola”

“Yule mwanamke mliyemteka usiku huu msibani. Yuko wapi? Aliuliza Ruby.

“Hayuko ha…….” alisema yule mwanamke. Ruby hakutaka mchezo,kwa kutumia kisu kile kikali alikata sehemu ya sikio na kumfanya agugumie kwa maumivu.

“Tuoneshe aliko Ambola ama nitakizamisha kisu katika shingo yako ! Alisema Ruby huku ncha ya kisu tayari ikianza kutoboa ngozi ya shingo.

“Yuko chumba namba 4. Chumba namba 4! Alisema yule mwanamke.

“Twende utupeleke” alisema Ruby na kumuinua mwanamke yule ambaye alikuwa anachechemea kutokana na jeraha la kisu katika paja lake. Huku akivuja damu aliwaongoza akina Ruby

hadi katika mlango ulioandikwa no 4. Ilihitajika kadi ya kuufungulia mlango huo.

“Fungua mlango haraka sana” aliamuru Ruby.

“Sina kadi ya kufungulia mlango huu” alijibu yule mwanamke. Bila kupoteza muda Jack alikisambaratisha kwa risasi kisanduku chenye mfumo wa kufungulia mlango ule. Aliupiga teke mlango ukafunguka wakaingia ndani na kumkuta Ambola

amejificha katika pembe ya chumba.

“Ambola please get up.” Alisema Ruby. Ambola alijitokeza akiwa anatetemeka.

“Are you okay? Hawajakuumiza hawa maharamia? Aliuliza Jack.

“Niko salama kabisa hawajanifanya chochote kibaya. Ahsanteni sana kwa kuniokoa. Ruby tuondokeni haraka mahali hapa. Jacob atarudi hapa muda wowote na akigundua nimemdanganya he will kill me” alisema Ambola.

“Ambola yuko sahihi. Tuondokeni. Vipi kuhusu huyu mwanamke?” aliuliza Jack.

“Huyu naye tunaondoka naye” alisema Ruby.

Jack alitangulia mbele akiwa na bastola akina Ruby wakamfuata nyuma. Walipofika sebuleni Ruby alichukua bastola ya yule mwanamke iliyokuwa mezani. Walitoka nje wakaelekea getini lakini kabla hawajalifikia,ulisikika muungurumo wa gari nje na

honi kupigwa. Walisimama na kutazamana.

“Wamerudi. Tutafanya nini? Aliuliza Ambola.

“Nendeni mkajificheni nyuma ya lile boksi la mbao. Mimi ninakwenda nje kumalizana nao. Gari letu liko njiani linazuia gari lao kupita. Ninakwenda kulitoa gari letu na mara tu wakatakapoingia ndani tutawashangaza” alisema Jack.

“Jack,hiyo ni hatari kubwa.” Alisema Ambola.

“Msihofu tafadhali. Lazima watahisi mimi ni mwenzao ndiyo maana nimekuja hapa. Tusipoteze muda nendeni mkajifiche” alisema Jack. Ruby aliwaongoza akina Ambola wakajificha nyuma ya boksi la mbao kama Jack alivyoelekeza.

Jack aliufungua mlango mdogo wa geti akatoka nje. Alikutana na watu wawili wakielekea getini.

“Hello guys” alisema Jack.

“Nini kinaendelea humo ndani? Kwa nini geti

halifunguliwi? Aliuliza jamaa mmoja.

“Gari hili lililoziba njia hapa ni la nani? Aliuliza mwingine.

“Samahani kwa usumbufu. Gari hili ni la kwangu. Nilitumwa mara moja kuleta mzigo Fulani ndiyo maana sikutaka kuingia ndani.” Alisema Jack huku akiingia ndani ya gari akaliwasha. Ililazimu gari la wale jamaa lirudi nyuma ili kulipisha gari la Jack. Jamaa wale wawili waliingia ndani wakitumia

mlango ule mdogo lakini nyumba ilitawaliwa na ukimya mkubwa.

“Hakuna mtu humu leo? Aliuliza jamaa mmoja mrefu mwembamba.

“Nashangaa” alisema mwingine huku wakipiga hatua kuelekea mlango wa kuingilia sebuleni.

“Hhhhhhhhhe…. !! Ilisikika sauti ya mtu. Yule mwanamke ambaye akina Ruby walikuwa wanamshikilia alitaka kupiga kelele lakini Ruby alimuwahi akamziba

mdomo. Ilitokea purukushani mwanamke yule alijitahidi kujitoa katika mikono ya Ruby. Sauti ile iliwafanya wale jamaa wawili kusimama na wote wakayaelekeza macho yao upande ule liliko boksi la Mbao.

Ilikuwa ni nafasi ya mwisho kwa mwanamke yule kujiokoa hivyo alijitahidi kwa kila namna awezavyo kupata nafasi ya kuchomoka lakini Ruby alikuwa imara kumdhibiti. Jamaa wale walisikia sauti za purukushani

ile nyuma ya boksi wakaamua kuelekea upande ule.

“Wanakuja upande huu” alisema Ambola. Ruby ambaye bado aliendelea kukabiliana na yule mwanamke hakutaka kupoteza muda alichomoa bastola akampigayule mwanamke risasi ya tumbo. Bastola ile haikuwa na kiwambo cha kuzuia sauti hivyo mlio wake uliwashitua wale jamaa wawili wakasimama na kila mmoja akachomoa bastola. Ruby alichungulia na kuwaona wale jamaa wawili wakiwa

wamesimama na bastola zao mikononi. Hakupoteza muda alijitokeza na kuachia risasi mfululizo. Jamaa wale wawili wote walikwenda chini.

Milio ya risasi kutoka ndani ya nyumba ile,iliwashitua jamaa waliokuwa garini wakisubiri geti lifunguliwe. Haraka haraka walishuka wakiwa na bastola mikononi ili kuelekea ndani. Ilikuwa ni fursa nzuri kwa Jack ambaye alishuka garini kwa haraka akaanza kucheza na bastola yake. Wale jamaa hawakutegemea

shambulio lile la ghafla. Jamaa watatu walianguka chini. Jamaa wawili waligundua risasi zilitoka nyuma yao katika bastola yenye kiwambo cha kuzuia sauti. Walijificha mbele ya gari lao na kuanza kuachia risasi kuelekea katika gari aliko Jack. Mmoja wao alichomoka na kukimbia kuelekea katika mlango mdogo wa geti. Mara tu alipoingia ndani alijibanza na kuanza kuachia risasi kuelekea garini aliko Jack ili kumzuia asipige risasi. Yule mwenzake

aliyebaki, alikimbia kuelekea katika mlango wa geti.

Ilisikika milio ya risasi mfululizo mle ndani walimokimbilia wale jamaa. Jack alipata hofu akakimbia kwa tahadhari hadi katika mlango wa geti. Aliupiga teke ukafunguka akajitoma ndani kwa tahadhari kubwa. Alishusha pumzi baada ya kukutana na Ruby na Ambola wakiwa karibu na geti.

“Hakuna wengine huko nje? Aliuliza Ruby. Tayari aliwamaliza wale jamaa wawili.

“Niliwaona watu watano wakishuka garini.Tumewamaliza wote” alijibu Jack.

“Tuondokeni haraka haraka. Milio hii ya risasi itawaleta polisi mahali hapa” alisema Ruby wakatoka nje.

“Kabla ya kuondoka tupekue gari lao kama kuna chochote tunaweza kukipata.” Alisema Ruby. Walifungua milango ya gari lile na wote wakapigwa na butwaa baada ya kumkuta mtu akiwa sehemu

ya nyuma hana fahamu amefungwa kamba.

“Thomas! alisema Ambola. Haraka haraka alishushwa akaingizwa katika gari la akina Ruby. Yule jamaa waliyemuua mwanzo alitupwa nje kisha Jack akaliondoa gari kwa kasi kubwa. Ruby alichukua kisu kutoka katika boksi la vifaa vya gari akazikata kamba zile alizofungwa Thomas. Ambola alikosa neno la kusema,machozi yalimporomoka.

“Ambola tafadhali nyamaza usilie. Karibu katika maisha yetu yaliyozungukwa na hatari nyingi. Pamoja na hatari tunazokutana nazo we don’t cry, ever” alisema Ruby.

“Ruby ninashindwa kujizuia kuangusha machozi. Siamini kama nimetoka salama kwenye mdomo wa Mamba. Jamaa tayari walikwisha nipata. Niliwaamini kile walichoniambia. Kama si ninyi leo ulikuwa ni mwisho wangu. Wamempata hadi Thomas Ngalula. Siri yangu tayari

wameifahamu. Ahsanteni sana Ruby kwa kuniokoa.” Alisema Ambola.

“Ambola unayepaswa kumshukuru ni Mungu,siyo sisi. Ni kwa maongozi yake ulipata wazo la kunipigia simu ukaufahamu ukweli.” Alisema Ruby.

“Nilikuwa tayari kumuuza Jack bila kujua. I’m sorry Jack.” Alisema Ambola.

“Hayo yamepita Ambola. Kwa sasa tujielekeze katika yajayo. Furaha yangu ni wewe kuwa mzima.” Alisema Jack.

“Kwa mara nyingine,ahsanteni sana jamani kwa hiki mlichokifanya usiku huu. Sikutegemea Ruby kama una uwezo mkubwa namna hii katika mapigano.”

“Mimi pia sikutegemea kabisa Ruby kama una uwezo mkubwa namna ile” alisema Jack.

“Nimekuwa karibu na Mathew kwa muda mrefu hivyo ninafahamu mambo mengi. Naomba ninaweke wazi kuwa mlima tunaopanda bado ni mrefu na kadiri tunavyozidi

kupanda ndivyo tunavyozidi kukutana na ugumu. Tunatakiwa tuwe na mioyo migumu kama jiwe. Tuko katika misheni moja na wanaume ambao huwa siamini kama wana mioyo tuliyo nayo sisi. Ni watu wa aina yake ambao sijawahi kujuta kuwafahamu. Ninawazungumzia Mathew Mulumbi na Gosu Gosu. Ni watu wa ajabu wasiochoka wala kukubali kushindwa. Hawalali usingizi hadi wahakikishe misheni imefanikiwa. Tunapaswa na

sisi tuwe majasiri kuwapa moyo kwa kufanya mambo kama haya tuliyoyafanya usiku huu.” Alisema Ruby.

****

Julius akiwa nje ya nyumba ya akina Ambola akimsubiri Jack, alizama katika tafakari ya kina. Wakati akitafakari ndipo alipokumbuka hakuichukua simu ya Ambola alipomaliza kuongea na Ruby.

“Nilifanya ujinga mkubwa sana kusahau kuichukua simu ile kwa Ambola. Ni vipi akiwapigia wenzake na kuwaelekeza mahali alipo? Aliwaza na haraka akachukua simu yake akampigia mmoja wa vijana wake waliobaki pale nyumbani akimlinda Ambola. Simu iliita bila kupokelewa. Alipiga simu ya mwingine lakini haikupokelewa.

“Kwa nini wote simu zao zinaita bila kupokelewa? Alijiuliza na kujaribu kwa mara nyingine tena kupiga lakini simu hazikupokelewa.

“Kuna kitu hakiko sawa.” Aliwaza Julius akawafuata wale walinzi wa kimasai akawataka wamjulishe pindi Jack atakaporejea.Haraka haraka aliingia garini na kumtaka dereva wake amrejeshe level I safe house. Alitaka kujua kwa nini vijana wake hawapokei simu.

Akiwa njiani aliwapighia simu watu wake ambao aliwataka wampeleke Thomas Ngalula level 1 safe house lakini nao pia simu zao ziliita bila kupokelewa.

“Nini kinaendelea huko? Kwa nini hawa nao hawapokei simu? Alijiuliza akaamua kumpigia simu Red.

“Boss” alisema Red baada ya kupokea simu.

“Red nini kinaendelea hapo? Kuna dalili zozote za Mathew Mulumbi kutokea?

“Mpaka sasa hakuna dalili zozote. Tunaendelea kusubiri” alijibu Red.

“Red misheni imeharibika. Sina hakika kama Mathew Mulumbi atatokea mahali

hapo. Mrudishe huyo mzee *safe house* tukutane hapo”alisema Julius na kukata simu halafu akapiga ofisini kwake SNSA.

“Zawadi tayari mmefahamu mahali anakojificha Mathew Mulumbi na wenzake? Aliuliza.

“Boss mpaka sasa bado hatujafahamu ila zoezi linaendelea.”

“Ugumu uko wapi Zaina kujua mahali walipo? Wameingia na kutumia mfumo wetu kwa nini msijue

walikuwa wapi wakati wanatumia mfumo wa SNSA?

“Boss,si jambo jepesi kwani hawa jamaa walitumia utaalamu wa hali ya juu sana kujiunga na mfumo wetu. Baada ya kuchunguza tumegundua walikuwa wanatumia mfumo wetu wakitokea kituo chetu cha zamani kilichopo Mzimu tete” alisema Zaina. Julius alikuna kichwa chake.

“Sawa Zaina endeleeni kufuatilia na pale mtakapopata

chochote mnijulishe haraka sana”

Alisema Julius na kukata simu.

“Nimepata jibu. Faraji ndiye aliyewasaidia hawa watu kujiunga na mfumo wetu. Ni yeye aliyefahamu kuhusu kile kituo chetu cha zamani cha Mzimu Tete. Amepata haki yake kwa usaliti mkubwa alioufanya. Hata hivyo tumekaribia sana kuwatia mikononi hawa washenzi wanaoumiza vichwa vyetu. Nina uhakika mkubwa

hawatamaliza usiku wa leo kabla hawajagundulika mahali walipo” aliwaza.

Julius alifika katika nyumba alikopelekwa Ambola. Kabla hajaifikia nyumba ile alishituka sana baada ya kuyaona magari ya polisi. Nje kulikuwa na umati wa watu.

“Kuna kitu kimetokea pale” alisema kwa wasi wasi. Alimtaka dereva wake wendeshe gari taratibu hadi walipoufikia utepe wa njano ambao ulifungwa na jeshi la polisi kuzuia watu na magari

kupita eneo lile ambalo lilifungwa kwa ajili ya uchunguzi. Julius alishuka garini akawafuata askari ambao walimtaka asogee mbali na eneo lile. Alitoa kutambulisho chake kinachomuonesha ni mkuu wa idara ya SNSA. Askari wale walibaki wanashangaa. Hawakuwa na habari kama kuna kitu kinaitwa idara ya siri ya usalama wa ndani wa nchi kifupi SNSA.

Mkuu wa kikosi kile cha askari aliitwa na kufahamishwa uwepo wa

mkuu wa idara inayoitwa SNSA. Naye pia alishangaa.

“Nini kimetokea hapa? Aliuliza Julius.

“Kuna mauaji yamefanyika usiku huu. Tulipata taarifa kutoka kwa wakaazi wa mtaa huu tukafika mara moja. Nani wanaishi humu? Aliuliza mkuu wa kikosi kile cha polisi. Julius alichanganyikiwa akachukua simu akampigia kamanda wa polisi kanda maalum ya Dar es salaam akamjulisha kuhusu kutokea kwa mauaji yale katika moja ya nyumba zao na

kumuomba awaondoe wale askari polisi ili idara yake iweze kufanya kazi ya uchunguzi wa tukio lile kwani liliwahusu wao. Mkuu wa timu ile ya askari alipigiwa simu na kamanda wa polisi kanda ya Dar es salaam akapewa maelekezo. Baada ya kupokea maelekezo naye aliwaelekeza askari wake kuipakia miili ya marehemu wote na kuipeleka hospitali kuhifadhiwa. Miili ilipakiwa haraka haraka katika gari moja la polisi kisha wakaondoka na kuwaacha

SNSA waendelee na uchunguzi wao.

“Kabla hajaingia ndani,Julius alimpigia simu Red akamtaka asimpeleke tena Gavana pale katika ile nyumba,akamuelekeza kumpeleka katika nyumba nyingine. Aliingia ndani taratibu akaelekea katika chumba alimokuwa amefungwa Ambola. Aliutazama mlango wa chumba kile ulivyoharibiwa kwa risasi. Alihisi mwili wake unaisha nguvu.

“Ambola ! Ambola ! alisema kwa hasira na kupiga ngumi ukuta.

“Aaaagghhh ! alisema kwa hasira halafu akapiga simu ofisi kuu ya SNSA akaagiza ifike timu ya uchuguzi haraka sana katika nyumba ile.

“Nitakupata Ambola. Huna kwa kukimbilia lazima utapatikana tu” alisema Julius kwa hasira.

****

“Hawa jamaa wameondoka kimya kimya sifahamu wamekwenda wapi. Niko njiani ninakuja kwako kuna jambo la muhimu mno nataka kukufahamisha.”

Lucy alirudia mara pili kuusoma ujumbe ule uliotoka katika simu ya Regina. Alitakari kwa sekunde chache halafu akaandika ujumbe wa majibu.

“I don’t think tha’ts a good idea Reg”

Baada ya sekunde chache ukaingia ujumbe mwingine kutoka kwa simu ya Regina.

“Picha yangu imesambaa kila kona ninatafutwa. Nitakapoonekana kila kitu kitavurugika. Nimekaribia sana kufika nyumbani kwako. Sintachukua zaidi ya dakika kumi”

“Sawa. Hakikisha umechukua tahadhari ya kutosha ili usionekane. Ni hatari sana ukionekana hapa kwangu. Tunaweza kuvuruga

mambo” Ulisomeka ujumbe wa Lucy

“Nimejificha nyuma ya gari. Naomba uwajulishe walinzi wako wasilikague gari hili ninalokuja nalo” ulisomeka ujumbe kutoka kwa Regina.

“*Gari gani unakuja nalo?* Aliuliza Lucy.

“Ni Range rover e vogue rangi nyeusi”

“Sawa nitatoa taarifa getini. Ukiingia ndani mwelekeze dereva asiegeshe

mbele ya nyumba bali azunguke nyuma aelekee katika bustani iliyoko nyuma,tutazungumzia huko. Hapa ndani kuna ndugu zake Gavana" ulisomeka ujumbe wa mwisho wa Lucy.

"Sawa" alijibu Regina.

Lucy mke wa Gavana alirejea sebuleni ambako ndugu wa Gavana walikuwa wamekusanyika wakisubiri kupata taarifa yoyote ya kupatikana kwa ndugu yao. Mpaka muda huo hakukuwa na taarifa yoyote kutoka kwa

vyombo vya usalama kuhusu kupatikana kwa Gavana.

Macho ya Lucy yaliikuwa mekundu kwa kulia. Kila alipotokea, ndugu waliokuwa sebuleni walihisi ana taarifa njema. Alizidi kuwavunja moyo alipowaambia hakuwa bado na taarifa zozote. Iliwalazimu ndugu wale kuanza maombi kumomba Mungu amsaidie ndugu yao. Regina naye alishiriki maombi yale. Wakati maombi yakiendelea aliinuka kimya kimya akazunguka nyuma ya nyumba akakaa katika pembe

moja iliyokuwa na mwanga hafifu.

“Sijapenda maamuzi haya ya Regina kuja hapa nyumbani. Anaweza akaniletea matatizo kama akionekana hapa. Eneo hili lina watu wengi leo na yeye tayari picha yake imesambaa kila sehemu anatafutwa na jeshi la polisi. Akionekana hapa atanisababishia matatizo makubwa.” Aliwaza Lucy.

Dakika tano baadaye mwanga wa taa za gari ulionekana.

‘Nahisi huyu atakuwa ni yeye Regina” aliwaza Lucy.

Gari lile lilizunguka nyuma ya nyumba na kuelekea moja kwa moja katika eneo la bustani. Baada ya taa za gari lile kuzima,Lucy alitulia kwa dakika mbili halafu akapiga hatua kuelekea bustanini. Alilifikia gari, mlango ukafunguliwa. Hakuwa na hofu yoyote alisogea hadi pale kwenye ule mlango uliofunguliwa akitegemea kumkuta Regina. Ghafla kwa kasi ya kimbunga alijikuta ameinuliwa na kusukumwa

ndani ya gari mlango ukafungwa. Mara tu alipoingizwa garini,alidakwa na mikono yenye nguvu akakabwa kabali hadi alipopoteza fahamu.

Taratibu gari liligeuzwa na kuondoka. Hakukuwa na tatizo lolote getini mara tu walipoliona gari lile walilifungulia mlango likatoka.

Mathew Mulumbi aliichukua simu ya Lucy akaizima na kutoa betri yake.

“Nimeupenda huu mchezo wa leo.” Alisema Gosu Gosu aliyekuwa katika usukani.

“Gosu Gosu bado ninauona mlima mrefu tunaotakiwa kuupanda. Mchezo ndio kwanza umeanza. Hawa jamaa wamejizatiti vilivyo kuhakikisha kila kitu chao kinafanikiwa. Niliuona ugumu wa mchezo huu baada ya kufahamu ndani yake yumo pia Israel Maungwana. Pamoja na ugumu wake lakini hatujawahi kukata tamaa katika misheni yoyote ile. Hatujawahi kushindwa. Hata

katika misheni hii hatutashindwa. Mungu yuko upande wetu kwani tunapambana kwa ajili ya taifa letu” Alisema Mathew.

“Mathew umekuwa ukiniambia mara kwa mara nisimuamini mtu yeyote. Katika tukio hili nimeamini usemi wako. Sikutegemea kabisa kama Regina anaweza akafanya hiki alichokifanya. Tumemuokoa na kifo lakini malipo yake ni haya.” alisema Gosu Gosu.

“Gosu Gosu hili suala linaonekana ni pana zaidi ya tunavyolifahamu. Kuna maswali magumu yanayohitaji majibu. Kwa kuwa tayari hawa wawili tunao,tutawahoji kwa kina na kufahamu kila kitu” alisema Mathew.

****

Mathew na Gosu Gosu walifika salama katika maficho yao. Lucy alishushwa garini akabebwa kunigizwa ndani. Ilikuwa ni furaha kubwa kwa

akina Ruby kuwaona tena akina Mathew.

“Ahsante Mungu mmerejea salama. Nilikuwa namuomba Mungu kila sekunde mrejee salama” alisema Ruby. Lucy alilazwa katika moja ya ofisi akaachwa humo ili azinduke.

“Tumerejea salama. Mambo yanakwendaje hapa? Nimeliona gari la Dr Philip hapo nje,wote mko salama humu? Aliuliza Mathew.

“Mathew tuko salama lakini kuna mambo yametokea” alijibu Ruby.

“Jombaa yuko wapi?

“Anamsaidia Dkt Philip kufanya upasuaji”

“Upasuaji? Mathew alishangaa.

“Ndiyo. Kuna mtu anafanyiwa upasuaji” alisema Ruby na kumuongoza Mathew hadi katika chumba alimo Dkt Philip. Aliusukuma mlango akaingia ndani na kumkuta Dkt Philip akinawa mikono.

Kitandani alilala mtu aliyekuwa bado katika usingizi.

“Hallow Dkt Philip” alisema Mathew.

“Mathew imekuwa vyema umekuja. Ninataka tu ufahamu kuwa hiki mlichokifanya leo sijakipenda hata kidogo. Nilitakiwa katika upasuaji muhimu sana wa mapacha walioungana lakini nikaitwa hapa kuja kumtoa mtu risasi. Mathew ninaanza kuchoshwa na haya mambo yako. Haupo tena katika shirika la ujasusi hivyo achana na mambo haya.

Wewe ni mfanya biashara kwa sasa. Waache majasusi wafanye kazi yao” alisema Dkt Philip. Mathew alimtazama kwa sekunde kadhaa na kusema.

“Dkt Philip wewe ni rafiki yangu,nakufahamu ni mzalendo lakini chunga sana usiweke fedha mbele ukaiacha nchi nyuma. Tunachokifanya hapa ni kwa ajili ya nchi na si kwa manufaa binafsi.”

“Mathew achana na kazi hizi. Umekwisha fanya sehemu yako waachie na wengine

wafanye sehemu yao. Pumzika. Unapoingia katika kazi hizi,wengi tunalazimika kukufuata pia. Unatuweka wote katika hatari" alisema Dkt Philip. Mathew alimtazama kwa makini na kusema.

"Iwe ni mara ya mwisho ulimi wako kutamka maneno kama hayo. Nikikusikia ukitamka maneno kama hayo tena mbele yangu nitaingiza risasi katika kichwa chako." Alisema Mathew na kutoka akimuacha Dkt Philip amesimama kama mlingoti.

Aliingiwa na hofu. Mathew aliwataka watu wote wakusanyike katika moja ya ofisi.

“Guys mambo yanazidi kupamba moto. Mimi na mwenzangu tumefanikiwa kumpata Lucy mke wa Gavana. Kuna mambo yametokea hapa wakati hatupo. Naomba taarifa tafadhali” alisema Mathew. Ruby alimweleza Mathew kila kitu kilichotokea wakati yeye na Gosu Gosu walipokwenda kumchukua Lucy. Ilimlazimu Mathew kupiga makofi

kuwapongeza akina Ruby kwa kile walichokifanya.

“Mnastahili pongezi za pekee kabisa kwa hiki mlichokifanya usiku huu. Natamani nchi nzima na dunia wangefahamu kile mlichokifanya usiku huu ili wafahamu uwezo wa mwanamke lakini kwa bahati mbaya tunafanya mambo haya kwa siri bila kujulikana. Narudia tena kuwapongeza kwa ushujaa huu mkubwa. Jack na Ruby hongereni kwa kumuokoa Ambola.” Alisema Mathew.

“Hongereni sana nyote kwa kazi nzuri” Gosu Gosu naye aliongeza.

“Tumepiga hatua kubwa sasa. Tumewapata watu muhimu sana ambao nina uhakika mkubwa tutapata mambo muhimu kutoka kwao. Tunaye Regina,vile vile tunaye mke wa Gavana ambaye alikuwa na mawasiliano na Regina. Tunaye pia mtu wa tatu ambaye ni yule jamaa aliyetoka kutolewa risasi. Pamoja na kufurahia mafanikio haya makubwa tuliyoyapata,siachi

kuwakumbusha kuhusu mlima mrefu tunaotakiwa kupanda. Hakuna mapumziko hakuna kulala hadi pale tutakapohakikisha tumeimaliza misheni hii" alisema Mathew na kumgeukia Ambola.

"Ambola wale jamaa walipokuchukua kuna maswali yoyote waliyokuuliza kuhusu sisi? Aliuliza Mathew.

"Hapana. Hawakuniuliza chochote. Nadhani kitu cha kwanza walichokuwa wanakihitaji ni kumpata Jack

pamoja na mtu wao. Nilimuamini yule jamaa kwa kuwa simfahamu. Niliamini kweli anafanya kazi na baba. Kama wangefanikiwa kumpata Jack pamoja na mtu wao ndipo ningejikuta katika matatizo makubwa." Alisema Ambola.

"Kwa ufupi tu ni kama alivyokueleza Ruby kuwa tayari hawa watu wamekufahamu unashirikiana nasi. Imekuwa vyema tumewahi kukuchukua kabla hawajapata chochote kutoka kwako. Kitendo cha kuua watu wao kadhaa ni tangazo la vita.

Wataongeza nguvu zaidi katika kutusaka. Hata hivyo msihofu.” Alisema Mathew.

“Mathew hizi taarifa za mzee Perfect kupigwa risasi ni taarifa za kweli? Aliuliza Gosu Gosu.

“Bado Dkt Philip hajaondoka anaweza kutusaidia kupata tarifa hiyo kutoka hospitali” alisema Mathew. Ruby alimfuata Dkt Philip katika kile chumba akamkuta akimpima Thomas Ngalula ambaye bado alikuwa usingizini.

“Huyu jamaa alichomwa dawa iliyomlaza usingizi. Itamchukua saa kadhaa hadi kuzinduka. Ukiacha haya majeraha madogo madogo, hana tatizo lingine kubwa” alisema Dkt Philip.

“Ahsante sana Dkt Philip. Mathew anahitaji kuzungumza nawe kwa dakika chache kabla hujaondoka” alisema Ruby na Dkt Philip aliongozana naye hadi katika chumba walimo akina Mathew.

“Dkt Philip,ahsante kwa msaada mkubwa na samahani

sana kwa kilichotokea. Endelea kutuvumilia kwani kazi hizi tutaendelea kuzifanya hadi siku tutakayoingia kaburini. Hatuna daktari mwingine tunayemtegemea zaidi yako. Tuachane na hayo,kuna taarifa ya kupigwa risasi jaji mstaafu Perfect Lyimo. Tunaomba utusaidie kuthibitisha taarifa hizi kama ni za kweli.” Alisema Mathew. Dkt Philip alichukua simu yake akampigia mtu Fulani wakazungumza kwa dakika mbili halafu akakata simu na kuwageukia akina Mathew.

“Ni kweli tukio hilo limetokea usiku huu. Jaji mstaafu Perfect amepigwa risasi na amefariki eneo la tukio. Mwili wake umehifadhiwa katika hospitali kuu ya Mtodora. Ambola alitazama chini. Taarifa ile ilimshitua sana.

“Ahsante Dkt Philip. Naomba usituchoke kila pale tutakapokuja kwako kuomba msaada” alisema Mathew. Gosu Gosu alimsindikika Dkt Philp hadi nje akaondoka.

“Pole sana Ambola kwa taarifa hii ya kifo cha Perfect Lyimo.” Alisema Mathew

“Pamoja na yote Perfect alikuwa mtu mwenye roho nzuri sana. Alinilea kwa upendo mkubwa tangu nilipotoka katika kambi ya wakimbizi.”

“Atakumbukwa kwa mazuri yake aliyoyafanya lakini kwetu atabaki kuwa msaliti wa nchi. Ambola naomba utafute ofisi moja ukapumzike. Sisi tunaendelea na kazi.” Alisema Mathew.

Ruby na Jack walimuongoza Ambola hadi katika ofisi moja akajipumzisha.Ruby alitoka akarejea kwa akina Mathew.

“Kabla ya kuanza kumuhoji Regina,Nataka Ruby uichunguze kwa kina simu ya mke wa Gavana. Nina uhakika mkubwa kuna mengi tutayapata kupitia simu hiyo.” alisema Mathew. Ruby aliichukua simu ya Lucy na kwenda kuanza kuichunguza.

****

Bilionea Charles Ombe alikuwa ametulia katika sebule yake kubwa akiwa na mawazo mengi. Ni muda mfupi baada ya kurejea kutoka katika kikao muhimu. Mke wake Martha ambaye hakuwa amelala akimsubiri mumewe, alimletea glasi ya mvinyo ambao Charles huupenda. Wakati mazungumzo yakiendelea sebuleni pale, simu ya Charles iliita. Alitazama mpigaji akaingiwa na hofu. Aliinuka akatoka sebuleni. Alitembea haraka haraka hadi katika

chumba kimoja kilichokuwa tupu akaingia na kuipokea ile simu.

“Mheshimiwa Rais” alisema Charles.

“Charles habari za usiku huu”

“Nzuri mheshimiwa Rais. Pole na majukumu”

“Ahsante sana. Nilikuwa natafuta nafasi nzuri nizungumze nawe mambo muhimu. Kubwa ni kuhusiana na operesheni inayoendelea. Nini kinaendelea? Ameuawa

Bernadetha,kabla hajazikwa anauawa tena mume wake. Usiku huu pia nimeambiwa yametokea mauaji katika moja ya nyumba za SNSA. Nini kinaendelea? Wewe ndiye mwenyekiti wa kamati kuu ya Tanzania mpya. Hebu nipe picha kwa upana nifahamu kinachoendelea kwa sababu na mimi ninaulizwa na wakubwa wangu halafu sina majibu ya kuwapa.” Alisema Dkt Nehemia Nchelela.

“Mheshimiwa Rais, muda mfupi uliopita nimetoka katika kikao cha dharura na kubwa

tulilolijadili katika kikao hicho ni hiki kinachoendelea sasa hivi katika operesheni yetu.”

“Ndiyo maana nimekupigia ili unieleze kwa kina kile kinachoendelea” alisisitiza Dkt Nehemia.

“Meshimiwa Rais ni kweli kuna matatizo yametokea. Kwanza kabisa tatizo lilianzia jijini Arusha. Naibu katibu mkuu wa chama cha ukombozi wa Afrika alitakiwa kuuawa. Aliyetumwa kwenda kufanya mauaji hayo ni kutoka kwa washirika wetu wa Congo. Kwa

bahati mbaya hakufanya kile alichoelekezwa kufanya. Aliharibu misheni.”

“Tuanzie hapo lilipoanzia tatizo. Ninataka kufahamu kwa nini alitakiwa kuuawa huyo naibu katibu mkuu wa chama cha ukombozi wa Afrika? Aliuliza Dkt Nehemia. ,

“Sababu ya kutakiwa kuawa ni baada ya kugundulika ana mawasiliano na baadhi ya vigogo ndani ya chama chako. Vile vile ilibainika kuwa ana mipango ya kuhama chama na kuhamia

katika chama chako. Sababu ya tatu ni baada ya kufahamu siri za ile kinachoendelea. Alishirikiana na dereva wa mwenyekiti wa chama kufanya uchunguzi kufahamu mipango yetu. Sababu hizo tatu ndizo zilizopelekea yafanyike maamuzi ya kumuua."

"Kwa nini ninayasikia haya leo? Aliuliza kwa ukali Dkt Nehemia.

"Mheshimiwa Rais,tulidhani itakuwa vyema tusikujulishe haya hasa baada ya kubaini siri zetu tayari

zimevuja na kuna watu wanatufuatilia. Hatutaki ijulikane kuwa nawe ni mmoja wa washirika wa mpango huu wa Tanzania mpya."

"Pamoja na hayo, lakini kukiwa na tatizo lazima nifahamishwe mapema kwa sababu na mimi wakubwa zangu wananiuliza. Tayari mmewafahamu hao vigogo ndani ya chama changu ambao huyo naibu katibu mkuu anashirikiana nao?

“Mpaka sasa bado hatujawafahamu tunaendelea kuwachunguza”

“Tatizo gani lilitokea baada ya mpango wa mauaji yake?

“Kama nilivyosema mheshimiwa Rais, aliyetumwa kwenda kufanya mauaji hayo ni kutoka kwa washirika wetu wa Congo. Kwa bahati mbaya mtu huyo hakufanya kile alichoagizwa akifanye na hakumuua Regina. Tatizo lingine ambalo liliibuka ni kwamba huyo jamaa

aliyetumwa kufanya mauaji hayo ni mshirika wa karibu wa mtu anaitwa Mathew Mulumbi ambaye amewahi kufanya kazi katika shirika la ujausi Tanzania”

“Mathew Mulumbi huyu mmiliki wa viwanda?

“Ndiyo mheshimiwa Rais. Yule ni mtu hatari sana. Amewahi kufanya kazi katika shirika la ujasusi kabla ya kuingia katika biashara. Huyo mtu aliyetumwa kufanya mauaji na Mathew ni washirika wakubwa hivyo

alimjulisha kuhusu mauaji hayo na ndipo Mathew Mulumbi alipojitokeza na tatizo lilianzia hapo. Mathew alimchukua Regina na mpaka sasa yuko naye. Tuna uhakika mkubwa tayari Regina amekwisha mweleza kuhusiana na mipango yetu. Huyu mtu akishirikiana na mtandao wake, tayari wamekuwa hatari kwetu na wanafanya kila wawezalo kuhakikisha mipango yetu haifanikiwi.”

“Nani aliyemuua Bernadetha? Ni hao akina Mathew Mulumbi?

“Kwa mujibu wa Julius ni kwamba Bernadetha aliuliwa na mmoja wa viongozi wa misheni ya Congo mpya anaitwa Joseph Tshibanga ambaye naye aliuliwa na mtu mwingine naye ni kutoka mtandao huo wa Congo mpya anaitwa Thomas Ngalula ambaye tayari imeaminika anashirikiana na akina Mathew Mulumbi. Tayari amefahamika mahali anakoishi na ninasubiri kupata

taarifa kutoka kwa Julius pale atakapotiwa mikononi.”

“Tulikosea sana kufanya mashirikiano na mtandao wa Congo mpya. Naona matatizo yote yameanzia upande wao. Hamkupaswa kumtumia mtu wa mtandao wao kwenda kufanya mauaji hayo Arusha. Nilifahamu mambo kama hayo yatakuwepo ndiyo mana niliiweka idara ya siri ya mambo ya ndani ya nchi chini yenu ili ihakikishe mambo yote yanakwenda vizuri. Kuna wataalamu wa hali ya juu sana ndani ya idara ya SNSA ambao

mngeweza kuwatumia katika kufanikisha mpango huo” alisema Dkt Nehemia.

“Mheshimiwa Rais ni kweli unalolisema lakini katika kikao tulichokaa kulijadili suala hili,zilitolewa sababu kadhaa kwa nini tumtumie huyo mtu wa upande wa Congo na wote tukakubaliana nazo. Mzigo wote wa lawama ninapaswa kubeba mimi kama mwenyekiti kwani nilikuwa na uwezo wa kukataa wazo hilo” alisema Charles.

“Lawama hazisaidii kitu chochote Charles zaidi ya kufanya mambo yawe magumu zaidi. Asubuhi nilipata taarifa za kutekwa kwa Gavana. Julius alinitumia ujumbe mfupi akanijulisha kuwa nisishituke kwa tukio hilo kwani ni wao ndio waliolifanya lakini hakutoa maelezo zaidi kwa nini wamefanya hivyo. Usiku huu nimepokea tena taarifa za kifo cha jaji mstaafu Perfect Lyimo. Muda mfupi uliopita nimepokea taarifa kutoka kwa mkuu wa jeshi la polisi Tanzania kuwa yamefanyika

mauaji katika moja ya nyumba za SNSA ambako watu wapatao saba wameuawa. Nimeshitushwa na mfululizo wa matukio haya ndiyo maana nimekupigia kufahamu nini kinaendelea?

“Mheshimiwa Rais,tukianza na suala la Gavana lilitokea alfajiri ya leo,iligundulika Gavana alikutana usiku na Mathew Mulumbi pamoja na Faraji Dilele”

“Gavana alikutana na Mathew Mulumbi na Faraji?

“Ndiyo mheshimiwa Rais”

“Nini sabau ya kukutana kwao? Mmekwisha fahamu mambo waliyoyazungumza? Aliuliza Dkt Nehemia.

“Mheshimiwa Rais, bado hatujui ni mambo gani wameyazungumza lakini inasadikiwa ni kuhusu suala la kupotea kwa mwanaye Kelvin.”

“Tangu amechukuliwa, amesema chochote?

“Mheshimiwa Rais,kitu kikubwa ambacho Julius na SNSA wamejielekeza ni kutaka

kufahamu mahali alipo Mathew Mulumbi. Gavana amekubali kutoa ushirikiano na hadi usiku huu bado wanaendelea na mipango ya kumsaka Mathew.”

“Charles suala hili la Gavana kutekwa halipaswi kuchukua muda mrefu kwani wananchi wataanza kuhoji vyombo vya ulinzi na usalama viko wapi? Jeshi la polisi wanaendelea kumsaka hivyo baada ya kuhojiwa anatakiwa aachiwe huru”

“Mheshimiwa Rais,katika kikao tulikubaliana kuwa Gavana baada ya kuhojiwa na kuonesha mahali aliko Mathew Mulumbi basi auawe”

“Auawe?

“Ndiyo mheshimiwa Rais”

“Hapana sitaki hilo litokee”

“Mheshimiwa Rais huyu mtu tayari amefahamu siri zetu na kama tutamuacha hai anaweza akaharibu kila kitu ndiyo maana tulikubaliana

kuwa baada ya kuhojiwa basi auawe”

“Charles tuliweke kwanza pembeni suala hilo tutalizungumza baadaye. Vipi kuhusu mauaji ya Jaji mstaafu Perfect Lyimo? Aliuliza Dkt Nehemia.

“Mauaji yale yamefanywa na SNSA”

“SNSA ndio waliomuua Perfect?

“Ndiyo mheshimiwa Rais.”

“Ni sababu zipi zilizopelekea wakachukua

maamuzi ya kumuua mtu muhimu kama yule?

“Mheshimwa rais,kuuawa kwa jaji mstafu Perfect hayakuwa maazimio ya kikao chochote bali ni jambo lililokuja kwa ghafla tu na kumlazimu Julius kufanya maamuzi hayo”

“Nataka kufahamu sababu za kumuua jaji Perfect”

“Sababu kuu ni kwamba Perfect amekuwa anatumiwa na akina Mathew Mulumbi ili kupata taarifa za mipango yetu. Tayari walikuwa

wameiunganisha simu yake na kompyuta yao na walikuwa wanafuatilia mazungumzo yake yote”

“Hiyo haiwezi kuwa sababu ya kuutoa uhai wa Perfect. Kama mligundua hivyo basi mngemjulisha na akatumia simu nyingine”

“Mheshimiwa Rais sijamaliza bado. Jaji Perfect alikuwa na mahusiano na Ambola binti ambaye amemlea tangu akiwa mdogo”

“Ambola? Dkt Nehemia alishangaa.

“Ndiyo mheshimiwa Rais.” Alisema Charles na kumpa Rais historia ya Ambola.

“Kwa nini Perfect alifikia hatua hiyo ya kutembea na huyo binti hata kama si mwanaye wa kumzaa? Mambo mengine tunayatafuta sisi wenyewe. Kwa nini alishindwa kutafuta mwanamke wa umri wake badala yake akaenda kutafuta huyo mtoto mdogo?

“Ambola kwa sasa ana umri wa zaidi ya miaka ishirini. Kilichomfanya Julius kuchukua maamuzi ya

kumuua Perfect ni baada ya kugundua Ambola anatumiwa pia na akina Mathew Mulumbi”

“Mathew Mulumbi again!

“Ndiyo mheshimiwa Rais.

“Kwa nini mmemuacha huyu mtu na mtandao wake wakapenya hadi kufika hatua hii? Nina uhakika mkubwa hata kama mmemuua Perfect lakini tayari kuna mambo mengi wamekwisha yapata kutoka kwake. Bernadetha alikuwa ni katibu huku Pefect akiwa msaidizi wake.

Wanafahamu kila kitu kinachofanyika. Lazima hao watu wamepata mambo mengi kutoka kwake”

“Kwa mujibu wa Julius,hao jamaa wameiunganisha simu ya jaji Perfect usiku huu kwa kumtumia Ambola. Baada ya Julius kupata taarifa hizo alichukua hatua za haraka sana kukata mawasiliano. Kingine alichokigundua ni kwamba tayari watu hao walikuwa wanatumia mfumo wa SNSA.”

“Wameingia hadi SNSA? Dkt Nehemia alizidi kushangaa.

“Ndiyo mheshimiwa Rais.” Alijibu Charles.

“Hapo ndipo ninapozidi kuchanganyikiwa. Wamewezaje kuingia katika mfumo wa SNSA?

“Mheshimiwa Rais,tunaamini wameweza kuingia katika mfumo huo kwa msaada wa Faraji Dilele.”

“Hili limenisikitisha sana. Watu wameweza kuingia

katika mfumo wa SNSA na kufanya wakitakacho bila wahusika kufahamu. Hii ni hatari kubwa kwa nchi. SNSA kuna siri kubwa za usalama wa ndani wa nchi yetu. Hawa jamaa wanapaswa watafutwe kwa udi na uvumba hadi wapatikane. Hawa watu ni hatari kwa usalama wa nchi ! alifoka Dkt Nehemia.

“Mheshimiwa Rais,juhudi za kuwaska zinaendelea na kwa mujibu wa Julius,ana uhakika usiku huu watafahamu mahali walipo”

“No! sitaki tena kusikia Julius akiendelea na operesheni hii. Umefanyika uzembe mkubwa sana hadi yakatokea haya yaliyotokea. SNSA ni idara kubwa haikupaswa kuchezewa namna hii. Sitaki kuzungumza sana lakini kuanzia sasa Julius si mkurugenzi tena wa SNSA. Nitatafuta mtu mwingine ambaye ataifanya kazi yake kwa weledi mkubwa.”

“With all due respect Mr President, I think that’s a mistake. Julius ameshiriki katika mchakato huu tangu

mwanzo. Kumuondoa sasa hivi tutakuwa tunafanya kosa kubwa mheshimiwa Rais”

“Hapana Charles. Ni kwa uzembe wa Julius tumefika hapa tulipo fika. Hii operesheni ni muhimu mno. Ni kitu pekee ambacho kitatuhakikishia sisi na familia zetu maisha mazuri huko mbeleni. Kama tukiharibu,tutakuwa tumeharibu pia maisha yetu. Nilikuwa kimya muda mrefu sikutaka kuwaingilia katika mipango yenu kwa kuamini mambo yanakwenda vizuri

kumbe mambo yanakwenda ndivyo sivyo. Nitampa nafasi hii mtu mwingine ambaye atahakikisha ndani ya muda mfupi ujao Mathew Mulumbi anapatikana. Kuanzia sasa nataka kila siku nipate taarifa ya namna mipango yote inavyokwenda. Kila mnachotaka kukifanya lazima kwanza kipate kibali changu. Ninafanya hivi ili kuhakikisha jambo hili linafanikiwa. Kuhusu Julius naomba usimweleze kitu chochote kwa sasa. Nitamweleza mimi mwenyewe! alisema Dkt

Nehemia kwa ukali na kukata simu.

“Niliamua kukaa kimya nikiamini kazi inafanyika kumbe ni upuuzi mtupu unaoendelea. Hii misheni ikikamilika itatuhakikishia maisha mazuri sana, endapo ikishindwa kukamilika tutakuwa katika hali mbaya. Huyu mtu ambaye ameteuliwa na chama changu kugombea urais akishinda uchaguzi sijui tutakimbilia wapi kwa mambo tuliyoyafanya. Nilipambana kuhakikisha chama hakimteui kuwa mgombea lakini

ilishindika kwani kila mjumbe alimtaka yeye. Njia pekee ya kujihakikishia usalama wangu na wenzangu ni kwa kuhakikisha chama hiki hakishindi uchaguzi mkuu badala yake kinaingia madarakani chama cha ukombozi wa Afrika. Nimekasirishwa na hawa watu tuliowaamini na kuwakabidhi jambo hili walisimamie namna wanavyofanya mambo kijinga. Utekaji na umwagaji mkubwa wa damu vitasababisha mipango yetu yote kuharibika. Tayari mpaka sasa watu

wameanza kuihusisha serikali na suala la kutekwa Gavana. Hii ni hatari kubwa kwetu" aliwaza Dkt Nehemia halafu akachukua simu yake akafungua sehemu ya kuhifadhia majina akalitafuta jina limeandikwa *I. Maungwana* akampigia. Simu iliita na kupokelewa.

"Mheshimiwa Rais."

"Israel habari za usiku huu"

"Njema kabisa mheshimiwa Rais. Pole na majukumu ya kuendesha nchi"

“Israel nimekupigia kuomba msaada wako”

“Nikusaidie nini mheshimiwa Rais?

“Nimebaini mambo yanakwenda ndivyo sivyo katika ule mradi wetu. Watendaji tuliowaamini kuwa wataifanya kazi hiyo kwa weledi wameanza kuvurunda na kama tusipokuwa makini tunaweza kuharibu kila kitu” alisema Dkt Nehemia na kumweleza Israel kila kitu alichoelezwa na Charles.

“Mheshimiwa Rais,mimi tayari nilikwisha ona namna mambo yanavyokwenda lakini sikutaka kusema kwa kuwa tulikubaliana sisi tukae kando na kuwapisha timu uliyoiteua wafanye kazi yao. Mimi nimejielekeza katika shughuli za chama nikitegemea upande wenu mambo yanakwenda vizuri kumbe yanafanyika mambo ya ajabu hadi kupelekea Mathew Mulumbi kufahamu mambo yetu. Ninamfahamu Mathew Mulumbi. Niliwahi kufanya naye kazi katika shirika la

ujasusi hapo zamani. Kama tayari amepenyeza mizizi katika mtandao wetu basi inahitajika kazi ya ziada kumuondoa. Sizungumzi kwa kukuogopesha bali kwa namna ninavyomfahamu Mathew Mulumbi. Ni mtu hatari kuliko kirusi.” Alisema Israel.

“Ndiyo maana nimekupigia simu kuomba msaada wako. Nataka unitafutie mtu mahiri anayeweza kuendesha idara ya SNSA kwa muda. Ninataka kumuondoa mkurugenzi wa sasa. Ni kwa uzembe wake

haya yote yametokea.” alisema Dkt Nehemia.

“Mheshimiwa Rais ninakupongeza sana kwa maamuzi hayo. Kuhusu mtu wa kuongoza SNSA hilo si tatizo. Kuna wataalamu wameingia nchini jana ambao wamekuja mahsusi kwa ajili ya ule mfumo wa tume ya uchaguzi. Hao wanafaa sana kuongoza SNSA kwa muda. Ni wataalamu wa hali ya juu sana katika mambo ya mawasiliano na udukuzi.”

“Israel,hapa tunazungumzia idara nyeti ya usalama wa ndani wa nchi. Idara kama hii haipaswi kuongozwa na mtu kutoka nje. Hatutaki watu kutoka nje wafahamu siri zetu. Nataka mzawa”

“Mheshimiwa Rais,wazawa ndio waliotufikisha hapa. Ninakushauri tuwatumie hao jamaa kutoka nje ni watalaamu wa hali ya juu sana. Wote wamewahi kufanya kazi katika shirika la ujasusi la Israel Mossad. Ni majasusi wabobezi.

Watatusaidia sana katika zoezi la kumsaka pia Mathew Mulumbi na mtandao wake. Baada ya zoezi hilo kukamilika tutafuta mtu ambaye ataongoza idara hiyo ila kwa sasa nakushauri tuwatumie hao jamaa. Majina yao ni Azriel Blank,Efrayim Cower na Moshe Herson. Hawa watasaidia hata kuboresha mfumo wa SNSA ili hao virusi watu wasiweze tena kuingia katika mfumo huo" alisema Israel.

"Israel una uhakika na hao jamaa?

“Nina uhakika mkubwa sana mheshimiwa Rais. Ni mimi niliyewapendekeza waje hapa nchini kwa sababu ninawafahamu.” Alijibu Israel.

“Sawa. Waandae watu hao ili kesho asubuhi nikawakabidhi ofisi waanze kazi mara moja”

“Usihofu kuhusu hilo mhesimiwa Rais. Nakuhakikishia utaipenda kazi yao na utatamani uwaajiri kabisa katika idara hiyo.” Alisema Israel.

“Israel nimekubali kwa sababu ninahitaji matokeo ya haraka sana. Tukifanya mchezo hata kidogo mambo yataharibika na tutakosa kila kitu. Hii ni misheni muhimu sana ambayo kama ikifaulu basi hatutalazimika kufanya kazi tena kujiingizia kipato katika maisha yetu yaliyobaki. Tumekaribia sana kuanza kuogelea katika bahari ya utajiri mkubwa hivyo yeyote anayehatarisha mipango yetu lazima aondolewe kwa gharama zozote zile,ndiyo maana nimekubali kuwaweka

wageni hao katika idara nyeti kama hii kwa usalama wa nchi" alisema Dkt Nehemia.

"Mheshimiwa Rais kuna jambo ligine ninataka kushauri ni la muhimu pia'

"Nakusikiliza Israel"

"Huyo jamaa ambaye unataka kumtoa katika nafasi yake ya uongozi wa SNSA ameshiriki katika kuanda misheni hii tangu mwanzo. Ukimuondoa sasa hivi lazima atakuwa na donge moyoni. Anaweza akawa kikwazo kwa

watu wataochukua nafasi yake.”

“Nini ushauri wako?

“Anapaswa auawe”

“Tumuue Julius?

“Ndiyo mheshimiwa Rais. Tukitaka tuendelee kuwa salama na misheni yetu iendelee vizuri lazima tumuue Julius. Tumeamua kufanya usafi hivyo basi yeyote ambaye anaonekana kuwa kikwazo kwetu lazima tumuondoe mara moja” alisema Israel.

“Israel damu nyingi tayari imemwagika mpaka sasa. Hatupaswi kuendelea kumwaga damu zaidi.”

“Mheshimiwa Rais umeamua wewe mwenyewe kuingia vitani. Kama kweli umeamua kuhakikisha operesheni hii inamalizika kwa salama basi lazima kuilinda kwa jasho na damu. Ninakuhakikishia mheshimiwa Rais, huyu jamaa lazima atakuwa kikwazo kwetu na njia peke ya kukiondoa kikwazo hicho ni kumuua. Kwa ajili ya misheni hii, yeye pia alifanya

maamuzi magumu ya kumuua hadi jaji mstaafu Perfect hivyo na sisi lazima tufanye maamuzi magumu ya kumuondoa tena usiku huu.”

“Dah ! unazidi kunichanganya Israel”

“Mheshimiwa Rais hili si jambo kubwa. Niachie jambo hili nilimalize haraka sana. Ninao vijana ambao wanaweza kuifanya kazi hiyo kwa ufanisi mkubwa. Just show me where Julius is right now” alisema Israel. Kilipita kimya.

“Mheshimiwa rais.” Aliita Israel.

“Israel umenipa wakati mgumu sana kuamua. Sikutaka Julius afe. Pamoja na uzembe mkubwa alioufanya hadi kuhatarisha operesheni yetu lakini bado ni kijana mzuri,msikivu na anayejituma”

“Mheshimiwa Rais,sahau kuhusu uzuri wake. Uzembe mdogo sana uliofanywa umesababisha mambo kufika hapa yalipofika. Kama si wewe kuamua kuingilia kati

unadhani nini kingetokea? Operesheni isingefanikiwa. Hilo lingekuwa anguko letu sote. Lazima kuwe na nidhamu kubwa katika kutekeleza misheni hii. Yeyote yule ambaye atafanya kosa hata dogo tu ahesabu hana uhai. Hii itasaidia watu kuwa makini. Mheshimiwa rais,zimetumika fedha nyingi sana kuandaa mpango huu hivyo tusikubali kushindwa kwa sababu ya mtu mmoja.” Alisema Israel.

“Sawa Israel. Naomba unipe dakika chache nifahamu mahali aliko Julius kisha

nitakujulisha” alisema Rais na kabla ya kukata simu akauliza.

“Hao wageni tayari wamekwisha anza kuufanyia kazi mfumo wa tume ya uchaguzi?

“Msiba wa Bernadetha ndio uliochelewesha mambo kuanza lakini tayari mwenyekiti ameandaa kikao kati ya hao wataalamu na mwenyekiti wa tume ya uchaguzi. Wanakutana usiku wa leo na kazi inaanza usiku huu huu” alijibu Israel.

“Good” alisema Rais na kukata simu.

Aliinamisha kichwa akazama katika mawazo.

“Nimuue Julius ! alizungumza peke yake.

“Ni kijana mtiifu na mchapakazi sana. Nilitaka nimpangie kazi nyingine lakini naona Israel yuko sahihi. Anaweza akageuka kikwazo kwetu. Ngoja tu nimuondoe kwani kwa uzembe wake operesheni imefika hapa ilipofika.” Aliwaza Rais na kufungua tena simu yake

akaitafuta namba ya Julius akampigia.

“Mheshimiwa Rais shikamoo”

“Marahaba Julius. Nataka kufahamu uko wapi sasa hivi? Aliuliza Dkt Nehemia.

“Niko level 1 safe hopuse. Yamefanyika mauaji ya watu wetu usiku huu mahali hapa. Niko na timu ya uchunguzi ya SNSA tunachunguza namna mauaji hayo yalivyofanyika”

“Naomba baada ya kumaliza uchunguzi huo

unijulishe kwa kina nini sababu za mauaji hayo” alisema Rais na kukata simu. Aliinamisha kichwa chini na kuendelea kuwaza. Bado suala la kumuua Julius lilimuumiza kichwa.

“Ngoja tu nimuondoe. Tunao vijana wengi mahiri ambao wanaweza kufanya kazi kwa ufanisi mkubwa” aliwaza na kwa kutumia simu yake aliingia katika mfumo wa SNSA lakini bado mfumo haukuwa umerudi. Aliingia katika mfumo wa dharura akachukua faili lenye ramani

na maelezo yote kuhusiana na nyumba zote salama za SNSA akamtumia Israel halafu akampigia simu.

“Julius yuko Level 1 safe house”

“Ahsante mheshimiwa Rais. Vijana wangu wako tayari na muda si mrefu wataondoka kuelekea huko. Nitakupa mrejesho kazi ikikamilika” alisema Julius na Rais akakata simu.

Dkt Nehemia alipiga hatua kutoka katika kile chumba lakini alipogusa kitasa

akakumbuka kitu . Aliichukua tena simu yake akampigia Charles Ombe.

“Mheshimiwa Rais”

“Charles kuna jambo ambalo ninadhani itakuwa vyema ukilifahamu moja kwa moja kutoka kwangu.”

“Ndiyo mheshimiwa Rais”

“Kwanza tayari nimekwisha pata watu watakaoongoza SNSA kwa muda. Ni wale wageni watatu ambao wamekuja kwa ajili ya kushughulikia mfumo wa tume

ya uchaguzi. Nimeambiwa tayari umeandaa kikao kati ya wale wageni na mwenyekiti wa tume.”

“Ndiyo mheshimiwa Rais. Tayari nimeandaa kikao usiku huu kati ya mwenyekiti wa tume na hao wageni. Hivi tuzungumzavyo tayari kikao kinaendelea” alisema Charles.

“Hao ndio watakaoongoza idara hiyo kwa muda hadi hapo tutakapompata mtu atakayefaa kuongoza. Nataka watu hao watusaidia pia katika zoezi la kumsaka Mathew

Mulumbi na mtandao wake. Tukiachana na hayo kuna jambo nataka ulifahamu. Nimesikitishwa sana na uzembe mkubwa uliofanywa na Julius. Kumtoa SNSA peke yake haitoshi,nimeamua kumuondoa kabisa”

“Samahani. Sijakuelewa mheshimiwa rais”

“Nini hujaelewa Charles? Nimeamua kumuondoa kabisa. Akiachwa hai atakuwa bado kikwazo kwetu. Haikuwa rahisi kufikia maamuzi haya lakini lazima niyafanye.

Nimeona ulisikie jambo hili kutoka kwangu mwenyewe. Funga mdomo wako asifahamu mtu” alisema Dkt Nehemia.

“Nimekuelewa mheshimiwa Rais,nashukuru kwa kunijulisha” alisema Charles na Dkt Nehemia akakata simu.

****

Julius Mukoke bado alikuwa na timu ya uchunguzi kutoka SNSA wakiendelea kuchunguza namna tukio lile la mauaji lilivyofanyika pale safe house level 1. Wakati wakiendelea na uchunguzi,simu ya Julius iliita. Hakusumbuka kuitoa mfukoni kwa kuwa alikuwa na kifaa cha kupokelea simu sikioni.

“Hallow” alisema Julius.

“Julius ni mimi Charles nimetumia namba nyingine kukupigia.”

“Charles samahani niliondoka kikaoni bila taarifa.Kuna dharura nililazimika k……” Alisema Julius na kukatishwa na Charles.

“Tuachane na hayo. Naomba unisikilize kwa makini Julius. Wewe ni kijana wangu. Tumekuwa pamoja tangu ilipoanza operesheni hii. Siko tayari kuona ukipotea”

“Una maanisha nini Charles? Aliuliza Julius.

“Nimetafakri sana lakini nimeamua kuvunja uaminifu

na kukueleza kile kinachoendelea. Julius naomba uondoke hapo ulipo haraka sana. Kuna watu wametumwa kuja kukuua”

Julius alihisi kama moyo wake unataka kuchomoka kwa namna ulivyobadili mapigo yake baada ya kupewa taarifa ile.

“Charles nani wanakuja kuniua? Nani kawatuma watu hao?

“Julius achana na kila unachokifanya sasa ondoka mahali hapo haraka sana.

Muda wowote watu hao watafika. Ninakujali kijana ondoka hapo haraka sana na usimuage mtu yeyote. Tafuta sehemu salama ukajifiche. Usimpigie simu mtu yeyote na hasa wa SNSA. Nimalizapo kuzungumza nawe zima simu yako na uondoke haraka sana mahali hapo" alisema Charles na kukata simu. Julius alivuta pumzi ndefu na kuzima simu yake. Taratibu alitoka nje na kuvuka upande wa pili wa barabara kisha akaanza kukimbia. Alikata kushoto akaufuata mtaa uliokuwa

kimya sana. Maeneo yale ni ya watu wenye uwezo mkubwa kifedha hivyo wakati ule kila mtu alikuwa ndani. Akitembea haraka haraka zilitokea gari mbili katika barabara aliyoiacha zikielekea mahali alikotoka. Alipata wazo akarudi nyuma akachungulia na kuziona gari zile zimesimama katika ile nyumba alikotoka.

“Ahsante sana Charles kwa kuniokoa.” Alisema na kutimua mbio. Hakusimama hadi alipofika katika baa moja ambako alikuta kuna teksi

mbili. Madereva teksi walipomuona walijua mara moja anahitaji huduma. Kila mmoja alimuita katika taksi yake. Julius aliingia katika taksi ya mwanzo na kumuelekeza dereva sehemu anakoenda. Jasho lilikuwa linamtiririka kwa sababu ya kukimbia na hofu ya kuuawa. Baada ya teksi ile kuondoka aligeuka nyuma kutazama kama kuna gari linawafuata. Alipojiridhisha hakuna gari linawafuata alishusha pumzi.

“Ahsante sana Charles kwa kuniokoa” alisema kwa sauti

ndogo ambayo dereva aliisikia.

,

“Brother una matatizo gani? aliuliza dereva

“Usinijali endesha gari” alisema Julius.

“Nani wanataka kuniua na kwa nini? Lazima nifahamu wanaotaka kuniua na sababu ya kufanya hivyo. Siwezi kukubali suala hili likapita kimya kimya. Lazima nifahamu” aliendelea kuwaza na kumuomba dereva simu yake ili ampigie mtu Fulani. Dereva alisita kutoa simu yake

baada ya kumuona Julius kama mtu aliyechanganyikiwa.

“Sikiliza ndugu yangu. Naomba nikueleze ukweli ili nikuondoe hofu. Unaniona niko katika hali hii ni kwa sababu nimefumaniwa na mke wa mtu nikafanikiwa kukimbia. Hata nguo zangu nimevalia barabarani. Naomba unisaidie simu nizungumze na mtu mara moja.” Alisema Julius na kuichomoa pochi yake akahesabu shilingi elfu sabini na kumpatia dereva yule ambaye aliziweka katika

mfuko wake wa koti halafu akampa Julius simu yake.

Haraka haraka Julius aliandika namba ya simu ya Charles akampigia.

“Hallow” alisema Charles.

“Charles ni mimi Julius. Ahsante sana kwa kunipa taarifa. Ahsante kwa kuniokoa”

“Nashukuru kama umetoka salama eneo hilo. Tafuta sehemu salama ukajifiche. Ninakushauri usikae tena hapa nchini.

Nenda nje ya nchi. Niko tayari kukusaidia katika hilo. Siwezi kukuacha”

“Nataka kuwafahamu watu wale ni akina nani? Nani amewatuma? Aliuliza Julius.

“Julius haitasaidia chochote kwa sasa hata kama ukifahamu. Kitu kikubwa kwa sasa ni kutafuta namna ya kuondoka hapa nchini na kwenda nje ya nchi.”

“Charles ninahitaji kufahamu tafadhali. Kama umeweza kunipa taarifa hii kubwa naomba unijulishe

tafadhali watu wale wametumwa na nani?

“Wametumwa na ngazi za juu”

Julius alishusha pumzi. Alihisi kutetemeka mwili hakuelewa ni hasira au ni woga.

“Una maanisha ni…. .” alisita kidogo.

“Julius ndiyo maana ninakwambia hupaswi kuendelea kukaa hapa Tanzania. Tayari ni sehemu hatari sana kwako.”

“Lakini kwa nini akafanya maamuzi haya? Kwa haya yote niliyoyafanya anawezaje kuthubutu kutaka kunifanyia kitendo kama hicho?

“Julius kitu cha msingi kwa sasa ni usalama wako. Haya mambo mengine tutazungumza siku nyingine. Kwa usiku huu tafuta sehemu salama ukajifiche. Hali imechafuka” alisema Charles.

“Nimekuelewa Charles. Kwa mara nyingine ahsante sana kwa kuniokoa” alisema Julius.

“Nimeona si haki kwa hiki anachotaka kukifanya. Umefanya mambo mengi na hustahili adhabu ya namna hiyo. Nakukumbusha tena usiiwashe simu yako wala usiwasiliane na mtu yeyote unayemfahamu”

“Nitafanya hivyo. Nawe pia chukua tahadhari kwani kitendo cha kunijulisha kuhusu hatari inayonikabili kitakuweka katika hatari kubwa” alisema Julius na kukata simu akamrudishia dereva simu yake.

“Sasa nimepata picha kwa nini Rais alinipigia simu na kuniuliza mahali nilipo. Kumbe alikuwa na mpango wa kufahamu nilipo ili atume watu kuja kuniua. Kwa nini amechukua maamuzi haya? Nimefanya jambo gani hadi achukue maamuzi haya na kwa wakati huu? Alijiuza.

“Ngoja nifuate ushauri wa Charles nitafute mahali salama nikajifiche usiku wa leo. Ninatakiwa kulitafakari kwa kina jambo hili na nini nifanye

baada ya kunusurika kifo. Natakiwa kufahamu kuwa mimi si wa thamani tena kwao na baada ya kunikosa watatumia kila njia kunisaka. Nitawaonesha kuwa wamekosea sana kutaka kuniua” aliwaza na kumueleza dereva sehemu nyingine anakotaka kwenda. Dereva alifuata maelekezo aliyopewa.

Walifika katika nyumba moja iliyozungushwa ukuta mkubwa. Julius alishuka na kumtaka dereva asimsubiri. Alielekea getini akabonyeza kengele geti likafunguliwa

akaingia ndani. Tayari alikuwa safe house 3.

“Red yuko wapi? Aliuliza Julius huku akikimbia kuelekea sebuleni ambako alimkuta Red ametulia akitazama filamu.

“Red,kuna mtu yeyote amekupigia simu akaniulizia?

“Hapana hakuna mtu aliyepiga simu”

“Good. Gavana yuko wapi?

“Yuko chumba namba moja” alisema Red huku akisimama na kuongozana na

Julius hadi katika chumba namba moja. Alikifungua chumba kile na kuelekeza Gavana afunguliwe akamshika mkono akamtoa ndani ya kile chumba.

“Nipe funguo za gari lako tafadhali” alisema Julius. Kisha pewa funguo alimuongoza Gavana wakaelekea katika gari la Red wakaingia.

“Boss kuna nini? Mbona hatuelewi kinachoemndelea? Aliuliza Red.

“Don’t wait for me. Go home ! alisema Julius na kufunga kioo cha gari. Geti tayari lilikuwa wazi akatoka kwa mwendo mkali na kuwaacha akina Red wakishangaa.

Mara tu alipoingia barabaani alizima kile kifaa ambacho kimefungwa katika magari yote ya SNSA ambacho kinaonesha mahali magari yote yalipo.

****

Watu wote walikuwa kimya ndani ya ofisi wakiwa wameyaelekeza macho yao kwa Ruby aliyekuwa anaikagua simu ya Lucy mke wa Gavana kama alivyoelekezwa na Mathew.

“Guys”aliita Ruby. Akina Mathew wakasogea mezani.

“Nimefanikiwa kupata ujumbe wote wa simu ambao Lucy ameutuma na kutumiwa kwa siku nzima ya leo. Kuna ujumbe alikwisha ufuta katika

simu yake lakini nimefanikiwa kuupata” alisema Ruby.

“Kazi nzuri Ruby. Tunahitaji kuwafahamu watu aliowasiliana nao ni akina nani na waliwasiliana nini.” Alisema Mathew.

“Ujumbe wa kwanza kwa siku ya leo umetoka kwa mtu anaitwa July. Huu ulitumwa saa kumi na moja kasoro.” Alisema Ruby na kuuufungua ujumbe ule.

“Ni taarifa ya kifo cha Bernadetha” alisema Ruby, na wote wakausoma ujumbe ule.

“Mauaji yamefanyika Safe house 6. Wameuawa watu 6 akiwemo mama Bernadetha. Gosu Gosu ametoweka. Anafahamu mengi ni mtu hatari sana kwetu. Tahadhari zichukuliwe kuanzia sasa. Mtajulishwa kile kinachoendelea. Julius”

“Ujumbe huu haukutumwa kwa Bernadetha peke yake. Ulitumwa kwa kundi” alisema Gosu Gosu.

“Ujumbe huu unatoa picha ya moja kwa moja kwamba

Lucy ni mshirika wa mtandao wa akina Bernadetha. Ukiona namna ujumbe huu ulivyoandikwa unawahabarisha kile kilichotokea katika nyumba yao salama.” Alisema Mathew.

“Baada ya kuupokea ujumbe huo,inaonesha Lucy alimpigia simu mtu anaitwa Julius. Kama SNSA wasingetuzimia mfumo wao tungeweza kupata rekodi walizungumza nini. SNSA wanahifadhi ya mawasiliano ya kila siku kutoka mitandao yote ya simu.” Alisema Ruby.

“Huyu Julius ni nani? Anaonekana ndiye mkubwa wao” alisema Gosu Gosu.

“Baada ya kuwasiliana na Julius kwa simu,dakika chache baadaye alituma ujumbe kwa huyo huyo Julius ukisomeka hivi *“He’s on move”* alisema Ruby.

“He’s on move” Gosu Gosu alirudia kuusoma ujumbe ule.

“Who was on move? Aliuliza Ruby.

“Hapa Lucy anampa taarifa Julius kuwa mtu huyo

ambaye ni wa jinsi ya kiume ameanza safari. Tujiulize ni nani? Kuna kitu kinazunguka kichwani kwangu sijui kama na ninyi mnawaza kama mimi. Gavana alitekwa alfajiri wakati akielekea kanisani katika ibada. Muda ambao unatajwa Gavana alitekwa na muda ambao Lucy alituma ujumbe kwa Julius unakaribiana sana. Hamdhani kuwa Lucy alikuwa anamjulisha Julius kuwa Gavana ameanza safari?

“Huyu ni mke wake wa ndoa,anawezaje akafanya

unyama wa namna hii? Gosu Gosu aliuliza.

“Hilo linawezekana. Zama hizi usaliti umekuwa mkubwa sana.” Alisema Ruby.

“Uwezekano ni mkubwa sana huyu mwanamke ndiye aliyetoa taarifa za Gavana kukutana nasi usiku kwa wenzake na kupelekea Gavana atekwe. Huyu ndiye aliyemuuza Gavana”

“Wanawake ! alisema Gosu Gosu huku akiuma meno kwa hasira.

“Endelea Ruby” alisema Mathew.

“Dakika ishirini tangu atume ujumbe ule wa *He’s on move* alitumiwa ujumbe mwingine na Julius ukisomeka *“we have him”*. Mathew yuko sahihi. Huyu mwanamke ndiye aliyemuuza mume wake. Baada ya ujumbe huo naye alituma ujumbe unaosomeka *“Remember don’t hurt him. Just question him and bring him back safe”*

Wote mle ndani walitazamana.

“Hadi mwili wote unanisisimka”alisema Gosu Gosu.

“Hakuna ubishi kuwa Lucy ndiye aliyefanikisha kutekwa kwa mume wake. Swali la kujiuliza kwa nini afanye hivi? Mume wake ni Gavana wa benki kuu ambacho ni cheo kikubwa kabisa. Yule mama anapata kila anachokihitaji lakini hajaridhika na akamzunguka mume wake akatekwa na kupelekwa katika mateso.”

“Nini wanachokitafuta kwake? Aliuliza Gosu Gosu.

“Naamini kikubwa wanachokitaka kwa Gavana ni kufahamu mahali nilipo. Kupitia mtu wao ambaye ni Lucy,tayari wamefahamu kuhusu mimi kukutana na Gavana jana usiku.” Alisema Mathew.

“Lucy pia alipigiwa simu na ile namba ya simu anayoitumia Regina. Ukitazama muda ni dakika chache baada ya sisi kuondoka

hapa kwenda msibani.” alisema Ruby.

“Jombaa,alimsikia akizungumza na mtu akimtaka amuonye mtu Fulani kuwa asiende msibani kwa kuwa jamaa wamekwenda huko. Kuna mtu alitakiwa kuonywa asiende msibani kwa kuwa tutakuwepo hapo kumfuatilia. Mtu pekee ambaye tulikuwa tunamfuatilia ni Israel Maungwana. Inawezekana alionywa mapema ndiyo maana hakutokea msibani siku ya leo” alisema Mathew.

“Wanawake ni watu wabaya sana” alisema Gosu Gosu.

“Si wanawake wote wabaya. Hapa tunawazungumzia hawa wanawake wawili. Lucy na Regina.” Alisema Mathew.

Waliendelea kuchambua ujumbe aliotuma na kutumiwaLuccy pia kufuatilia simu alizopiga na kupigiwa. Ujumbe wa mwisho ambao Regia alimtumia Lucy ni ule aliomjulisha kuwa akina Mathew tayari

wameiunganisha simu ya Perfect na kopyuta yao na walikuwa wanafuatilia mwasiliano yake. Sekunde chache baada ya kuupokea ujumbe huo,Lucy alimpigia simu Julius.

“Huo ulikuwa ni ujumbe wa mwisho ambao Regina alimtumia Lucy siku ya leo. Baada ya ujumbe huo Lucy alimpigia simu Julius. Nadhani alimpa taarifa hizo na ndipo ghafla mawasiliano na simu ya Perfect yalipotea. Nadhani ni wakati huo aliuawa” alisema Mathew.

“Mathew unadhani waliomuua jaji Perfect ni wenzake? Gosu Gosu aliuliza.

“Sina uhakika bado lakini aliuawa baada ya kubainika mawasiliano yake yanafuatiliwa. Jambo lingine,kupitia kwa Regina waliweza kumfahamu Ambola ni nani. Picha hizi mbili zinamfanya jaji Perfect aonekane ni hatari kwa mtandao na yawezekana aliondolewa ili kuondoa hatari. Tutafahamu zaidi baada ya uchunguzi” alisema Mathew.

Walitazamana kwa muda halafu Mathew akasema.

“Mpaka hapa hatuna shaka kuwa Lucy ni mshirika wa mtandao wa akina Bernadetha. Regina naye anashirikiana na Lucy. Swali. Je Regina naye ni mshirika wa mtandao huo? Kama ni mshirika wao kwa nini walitaka kumuua? Aliuliza Ruby.

“Kama nilivyosema kuna jambo bado hatulifahamu kuhusu Regina. Ruby naomba nakala ngumu za mawasiliano

yote ya Regina na Lucy” alisema Mathew.

Haraka haraka,Ruby alitoa nakala ngumu akampatia Mathew.

“Ni muda wa kuufahamu ukweli. Yawezekana tutakachokisikia kinaweza kubadilisha mchezo mzima.”

“Mathew naomba unipe dakika kumi tu nikaseme na yule mwanamke. Nina uhakika ndani ya muda huo atasema kila kitu” aliomba Gosu Gosu.

“Gosu Gosu ninafahamu bado una hasira na Regina kwa kile alichokufanyia. Hii si nafasi ya kulipiza kisasi” Alisema Mathew huku akitoa kicheko cha chini chini akatoka katika ile ofisi akaenda katika chumba alimo Regina. Jombaa alikuwa mlangoni kuhakikisha Regina anakuwa salama.

“Jombaa ahsante sana kwa kazi nzuri. Tusingefika hapa tulipofika bila wewe. Nenda kapumzike.” Alisema Mathew lakini Jombaa alionekana kuna

kitu anahitaji kuzungumza na Mathew.

“Jombaa nafahamu kuna kitu unataka tuzungumze lakini tutapata wasaa baadaye kidogo tutazungumza kwa kina. Nenda kapumzike”

Mathew aliufungua mlango wa ofisi alimo Regina ambaye alikuwa amefungwa barabara katika kiti. Alimtazama halafu akaufungua waya aliofungwa Regina,akavuta kiti akaketi. Alitumia sekunde kadhaa akimtazama usoni kwa makini.

“Don’t you have something to say? Aliuliza Regina.

“Imenilazimu nikutazane kwanza kwa makini sana kwa sababu mambo uliyoyafanya sikuyatarajia.” Alisema Mathew na kuweka kituo akaendelea kumtazama Regina ambaye alianza kutazama chini.

“Ulitaka kuuawa. Ni sisi tuliookoa maisha yako. Tuko katika hali ngumu hivi sasa,tunasakwa kila kona ya nchi kwa sababu yako. Tayari tulianza kukuamini na

kukushirikisha katika timu yetu kumbe tulikuwa tunafuga Nyoka mwenye sumu kali ambaye ametugeuka na kutugonga wenyewe. Regina nimekuja kuzungumza nawe kwa kutumia lugha laini nataka kukufahamu wewe ni nani na kwa nini ukafanya haya uliyoyafanya. Are you a spy? Aliuliza Mathew. Regina hakumjibu kitu bado aliendelea kutazama chini.

“Nilitazama namna ulivyomuelekezea Gosu Gosu bastola. You look professional. Tuachane na hilo turudi katika

swali langu nililokuuliza. Who are you? Tell me the truth" alisema Mathew na kugeuka baada ya kuwaona Gosu Gosu na Ruby wakiwa nje ya chumba kile wakifuatilia kile kinachoendelea. Mlango wa ofisi ile ulikuwa wa kioo. Bado Regina hakujibu kitu.

"Regina zungumza nami tafadhali. Ni mimi Mathew Mulumbi niliyekutoa Arusha na kukuleta hapa Dar es salaam. Don't you have something to say to me?

Regina aliinua kichwa akamtazama Mathew halafu akakiinamisha tena.

“Regina, si kawaida yangu kubembeleza mtu azungumze nami hasa kwa wakati kama huu lakini kwako nimelazimika kujishusha na kukubembeleza uzungumze nami kirafiki na unieleze kila kitu kuhusu wewe. Kama ukishindwa kunieleza mimi,kuna mtu yuko hapo nje anasubiri nimuite aingie humu ndani. Nakuhakikishia akiingia humu ndani utazungumza kila kitu lakini hadi wakati huo

hautakuwa ukitazamika. Ni kiumbe asiye na huruma hata kidogo. Mimi sitesi wanawake lakini yeye hajali wewe ni mwanamke au mwanaume anatesa watu wote. Ni afadhali ukakutana na Simba unaweza kutokea muujiza akakuacha lakini kwa Gosu Gosu hakuna muujiza. He's a Monster. Mbaya zaidi tayari umeharibu baada ya kutaka kumuua. Nakuhakikishia nikimruhusu aingie humu utazungumza lugha hadi zile usizozijua. Tafadhali usiipoteze nafasi hii. Talk to me" alisema Mathew.

Regina aliinua kichwa akatazama mlangoni ni kweli alikuwa amesimama Papi Gosu Gosu. Sura ake ilionesha hasira. Ni wazi aliisubiri sana kupata fursa ile ya kuingia mle ndani kuzungumza na Regina.

“Regina ninakuomba kwa mara ya mwisho,zungumza nami tafadhali. Usihofu hakuna anayetusikiliza huko nje. Hakuna kamera hakuna kifaa chochote cha kurekodi. It’s just us. You and me” alisema Mathew.

“Ni…”alisema Regina na kukohoa kidogo.

“Nimeshakueleza kila kitu kuhusu mimi, sina cha kukueleza zaidi.” alisema Regina.

Mathew aliiweka mezani nakala ngumu ya mawasiliano ya Regina na Lucy. Ujumbe wote waliotumiana ulikuwa katika karatasi ile.

“Soma hiyo karatasi” alisema Mathew. Regina aliichukua karatasi ile akaisoma na kuitupa mezani.

“Karatasi hiyo ni ushaidi tosha kuwa mimi nawe bado tuna mengi ya kuzungumza. Tuanzie katika ile simu. Where did you get it? Aliuliza Mathew. Regina hakujibu.

“Tulipotoka Arusha hukuwa na simu. Hii uliyoitumia kuwasiliana na Lucy uliipataje? Aliuliza Mathew. Midomo ya Regina ilicheza kama vile anataka kuzungumza lakini alisita.

“Regina,muda si rafiki kwangu. Naomba uokoe muda wangu unieleze kile

kinachokihitaji. Ndani ya dakika chache zijazo kama hutafunguka,ataingia humu Gosu Gosu. Ninakuhakikishia utaomba ugeuke ndege upae lakini haitawezekana. Nafasi hii uliyoipata usiipoteze. Nieleze ukweli bila kunificha kitu chochote" alisema Mathew.

Regina alionekana kutaka kusema kitu lakini alisita. Mathew aliinuka.

"Dirisha limefungwa. Nafasi uliyoipata umeshindwa kuitumia. Nitarudi hapa

baadae” alisema Mathew na kupiga hatua kuelekea mlangoni akaufungua akamuita Gosu Gosu.

“Gosu Gosu nakukabidhi mtu huyu. Hakikisha anasema ukweli. Baada ya dakika kumi nitarejea”

“Dakika kumi nyingi Mathew. Rejea baada ya dakika tano utakuta kila kitu mezani” alisema Gosu Gosu. Regina aliingiwa na hofu kubwa baada ya kumuona Gosu Gosu.

“Mathew ! aliita Regina. Mathew aligeuka akamtazama.

“Mtoe huyu mtu humu ndani”

“Uko tayari kueleza kila kitu? Aliuliza Mathew.

“Nitakueleza kila kitu.”

“Are you sure?

“I swear. Nitakueleza kila kitu.” Alisema Regina.

“Good. Gosu Gosu naomba dakika chache” alisema Mathew na Gosu Gosu akatoka nje.

“Tafadhali naomba usipoteze tena wakati wangu. Tuanzie katika ile simu. Where did you get it?” alisema Mathew. Regina alivuta pumzi ndefu. Nafsi yake ilionekana kuumizwa na kile anachotakiwa kukisema. Mathew aliligundua hilo.

“Usigope Regina. Nieleze kila kitu” alisema Mathew.

“Nitakueleza kila kitu lakini nataka tufanye makubaliano”

“Nini unakihitaji? Aliuliza Mathew.

“Nataka unisaidie niondoke hapa nchini. Kama unakubaliana na sharti hilo nitakueleza kila kitu.”

“Kwa nini unataka kuondoka nchini?

“Kwa sababu nitakufa kama nitaendelea kukaa hapa nchini” alisema Regina.

“Regina nimekwisha kuhakikishia hakuna atakayekuua ukiwa katika mikono yetu. Nimekuahidi ulinzi” alisema Mathew.

“You don’t understand. You can’t protect me from them. Thay’re powerfull than you” alisema Regina.

“Ni akina nani hao? Nieleze tafadhali” alisema Mathew. Kilipita kimya cha sekunde kadhaa,Regina akasema.

“Tukiwa Arusha……” Regina alisema na kusita.

“Endelea” alisema Mathew.

“Niliomba mnipe simu nizungumze na mume wangu.

Ukweli mimi sina mume. Niliyetaka kuzungumza naye ni Innocent Sungura yule jamaa ambaye tayari umekutana naye”

“Ndiyo nimekutana naye”

“Yule ndiye aliyenipatia simu.”

“Naye yumo katika mtandao wenu? Aliuliza Mathew. Regina akatikisa kichwa kukataa.

“Naamini simu hiyo ilikuwa kwa ajili ya kufanya

mawasiliano na watu wako akiwemo Lucy.”

“Ndiyo. Nilihitaji kujua kwa nini nimetaka kuuawa?

“Lakini hukuwasiliana na mtu mwingine yoyote zaidi ya Lucy”

“*She’s the only one I trust*”

“Katika mawasiliano yote uliyowasiliana na Regina ulikuwa unampa taarifa za kile tunachokifanya hapa. Why? aliuliza Mathew. Regina hakujibu.

“Regina unavyokaa kimya ni dalili ya kiburi na mimi sipendi watu wenye kiburi. Utanieleza au nimuite Gosu Gosu uzungumze naye?

“It’s because you are about to blow up our mission” alijibu Regina.

“Misheni ipi hiyo? Aliuliza Mathew. Regina aliaki kimya.

“Nakuuliza Regina ni misheni ipi hiyo ambayo tunataka kuiharibu?

“You won’t understand! Alijibu Regina.

“Make me understand! Alifoka Mathew. Regina alinamisha kichwa chake.

“Regina nataka ufahamu kuwa tayari tunaye Lucy Mzumile mke wa Gavana ambaye ulikuwa unawasiliana naye. Tumeichunguza simu yake tukagundua kila ulipompa taarifa zetu naye aliwasiliana na mtu anaitwa Julius. Kwa ushahidi tulioupata hadi sasa hakuna shaka Lucy Mzumile ambaye ulikuwa unawasiliana naye ni mshirika wa akina Bernadetha. Kama Lucy ni mshirika wa

mtandao huo,lazima wewe nawe unashirikiana nao. Kama unashirikiana nao kwa nini walitaka kukuua? Aliuliza Mathew.

“Mimi sina ushirika na mtandao wa akina Bernadetha” alijibu Regina.

“Soma ujumbe uliomtumia Lucy. Hakuna shaka wewe nawe ni mmoja wao.”

“Mimi si mmoja wao” alisema Regina.

“Ulifahamu tulikuwa tunakwenda msibani

kuchunguza kama Israel Maungwana atafika msibani hapo. Baada ya sisi kuondoka ulimpigia simu Lucy ukamjulisha kuwa tumeondoka na ukamtaka amjulishe mtu Fulani asiende msibani kwa sababu tunakwenda hapo. Nani uliyemtaka Ruby amfikishie ujumbe ili asifike msibani? Aliuliza Mathew. Uso wa Regina ulionesha mshituko mkubwa.

“Regina nasubiri jibu. Nani uliyemuonya kuhusu sisi kuwepo msibani hapo? Aliuliza

tena Mathew. Regina hakujibu. Aliinamisha kichwa chini.

“Labda nikusaidie kujibu. Ulifahamu kuwa tunakwenda msibani pale kuchunguza kama Israel Maungwana atafika. Lengo letu ni kutafuta mahusiano kati ya Israel na akina Bernadetha. Ulimtaka Lucy amuonye Israel asifike pale msibani kwa kuwa tutakuwepo.” Alisema Mathew na kumkazia macho Regina ambaye bado aliinamisha kichwa chini.

“Ukimya huo unanifanya niamini hiki nilichokisema ni kitu cha kweli. Kama ndivyo kwa nini ulitaka tusifahamu kama Israel Maungwana ana mahusiano a akina Bernadetha? Awali ulisema kuwa chama chako ndio wanaotaka kukuua baada ya kufahamu siri zako lakini unageuka na kumkingia kifua mtu aliyetaka kukuua. Hapo ndipo panapotuchanganya hata sisi. Naomba utuweke wazi tafadhali kwa nini unashirikiana na watu wanaotaka kukuua? Aliuliza

Mathew. Regina hakuonesha dalili zozote za kutoa jibu. Mathew akainuka.

“Regina nilikuonya tangu mapema kuwa sihitaji mtu wa kunipotezea wakati wangu. Tayari nilianza kushawishika kukusaidia kutoka hapa nchini baada ya kuamua kunieleza ukweli lakini ghafla umegeuka bubu. Kwa kuwa umepoteza muda wangu na hutaki kuongea nakwambia hutaondoka hapa nchini na utazungumza kila kitu mbele ya Gosu Gosu” alisema Mathew huku akiinuka.

“Mathew naomba uketi tafadhali” alisema Regina.

“Regina ninakuonya. Hii itakuwa ni mara ya mwisho na ukithubutu kunipotezea wakati wangu sintakuwa na huruma nawe tena” alisema Mathew.

“Tafadhali kaa tuzungumze. Sitaki unikutanishe na yule jamaa” alisema Regina.

“Haya zungumza” alisema Mathew.

“Ninahitaji sana kuondoka hapa nchini kwenda mahali

ambako nitakuwa salama. Kwa sasa nimekwama na siwezi kuondoka hapa nchini bila msaada wako. Ninakushukuru ulinisaidia kuondoka salama Arusha naomba uendelee kunisaidia" alisema Regina.

"Regina nitakusaidia kama utachagua kunieleza ukweli. Nikiona kile utakachonieleza kina manufaa nitakusaidia kuondoka hapa nchini kwenda mahali salama. Uchaguzi ni wako kama uko tayari kuondoka hapa nchini au ubaki." Alisema Mathew.

“Nitakueleza ukweli wote ila kumbuka umekwisha ahidi kunisaidia naomba utekeleze ahadi yako.”

“Uwezo wa kukusaidia ninao. Nataka maelezo” alisema Mathew. Regina alivuta pumzi ndefu.

“Mathew suala hili ni pana zaidi ya unavyolifikiri” alisema Regina akaweka kituo.

“Ndiyo maana ninataka unieleze kila kitu ili nilifahamu jambo hili kiundani” alisema Mathew.

****

Gavana wa benki kuu Jackson Mzumile mwili ulimtetemeka akiwa ndani ya gari la Julius. Hakujua anapelekwa wapi. Julius alikuwa ameloa jasho na aliendesha gari kwa kasi. Tangu walipoondoka katika ile nyumba alimokuwa amefungwa Gavana,Julius hakuongea neno lolote.

“Huyu jamaa ananipeleka wapi? Nahisi ndiye mkubwa wa wale jamaa. Mbona

haniulizi chochote? Nahisi anakwenda kunimaliza baada ya kugundua nimewadanganya. Ni kweli niliwadanganya wale jamaa nilikuwa na miadi ya kukutana na Mathew Mulumbi usiku huu. Tumekaa zaidi ya saa mbili katika daraja tukimsubiri Mathew Mulumbi. Safari hii hakuna msamaha. Huku tuendako sintarudi salama. Natamani kabla ya kuuawa ningepata nafasi ya kumuaga mke wangu Lucy.” Aliwaza Gavana.

“Lakini mbona hajanifunga pingu mikononi kama wale vijana wake? Gavana alijiuliza swali huku akiendelea kumtazama Julius ambaye alikuwa makini katika usukani huku bastola yake ikiwa mapajani.

“Kila nikitafakari kwa nini Rais atake kuniua ninakosa jibu. Tangu nimeingia SNSA nimeifanya kazi yangu kwa weledi mkubwa. Hakuna maelekezo aliyowahi kuyatoa nikashindwa kuyatekeleza. Kila kazi aliyonipa niliitekeleza kwa weledi mkubwa. Alinipatia

pia jukumu lingine la kuhakikisha SNSA inatumika katika kufanikisha mpango wa Tanzania mpya. Nimelibeba jukumu hilo kwa weledi mkubwa pia hadi tumefika hapa. Ni bahati mbaya tu imetokea mambo yameharibika baada ya akina Mathew kuingia na hii yote ni kwa sababu ya ubishi wa viongozi wa kamati ya Tanzania mpya. Je Rais anataka kuniua kwa ajili ya jambo hilo? Aliwaza Julius.

“Hapana huu ni uonevu mkubwa kabisa. Nimefanya

mambo mengi makubwa,nimefanya kazi zao nyingi za siri nyingine za mauaji. Sijawahi kufumbua mdomo wangu mahali popote nikaeleza yale maovu yanayofanywa na viongozi. Kwa kuwa wameamua kuniua na wamenikosa,kinachofuata ni mimi na wao. Charles amenishauri nikimbie niende nje ya nchi. Ushauri wake ni mzuri kwa kuwa anafahamu nikiendelea kukaa hapa nchini lazima nitauawa. Pamoja na hatari hiyo ya kuuawa siwezi kukimbia nchi. Nitabaki hapa

nchini. Kwa kuwa wameamua vita,nitapambana nao. It's me and them. Kama ni kufa ni bora nife nikipambana kuliko kukimbia nchi. Nitapambana" aliwaza Julius.

Baada ya mizunguko kadhaa, hatimaye gari lilisimama katika baa moja. Mara tu gari liliposimama makahaba wanne walilisogelea wakidhani ni mteja anahitaji huduma. Julius alimtazama Gavana ambaye hakuelewa kwa nini walikuwa mahali pale.

“Ondoa hofu Gavana. Uko salama” alisema Julius. Kauli ile ilimshangaza kidogo Gavana. Japo ilimuondoa kidogo hofu aliyokuwa nayo lakini ilimuacha na maswali kichwani. Julius alifungua sehemu katika gari akatoa kofia na miwani myeusi akampa Gavana avae. Baada ya Gavana kuvaa kofia na miwani,Julius alichomoa pochi yake akatoa noti ya shilingi elfu kumi akashusha kioo kidogo.

Kahaba mmoja alijizungusha na kumuonesha

Julius namna alivyopendelewa umbo lenye mvuto wa aina yake. Julius alimpa ile noti ya hilingi elfu kumi.

“Niiitie Tina pale kaunta” alisema Mathew na yule mwanadada aliondoka haraka kuelekea ndani. Hakutegemea kama angeweza kupata pesa ile kirahisi namna ile. Gavana alimtazama Julius halafu akakohoa kidogo na kusema

“Najua lengo lenu ni kuniua lakini naomba kabla ya kuniua unipe walau sekunde kumi tu nimuage mke wangu”

alisema Gavana huku sauti yake ikiwa na kitetemeshi.

“Kuwa na amani. Hakuna atakayekuua. Kama ingekuwa ni kukuua hivi sasa tayari ungekwisha uawa” alisema Julius.

Dirisha la upande wa dereva liligongwa,Julius akashusha kioo kidogo.

“July. Mbona leo huingii ndani? Aliuliza yule mwanamke aliyeitwa.

“Tina nina haraka nitakuja baadaye. Ninaomba chupa

mbili za maji ya kunywa.” Alisema Julius na kumpatia mwanamke yule shilingi elfu ishirini. Baada ya muda mfupi mwanamke yule alirejea akiwa na chupa mbili za maji ya kunywa akampatia Julius wakaagana akapandisha kioo cha gari na kumpatia Gavana chupa moja ya maji. Julius aliiweka mdomoni ile chupa ya maji na alipoishusha haikuwa na kitu. Aligeuka akamtazama Gavana.

“Mzee naomba ondoa hofu. Nimekutoa mahali pale hauko tena katika hatari.”

Alisema Julius. Kilipita kimya cha sekunde kadhaa halafu akasema.

“Naitwa Julius Mukoke. Ni mkurugenzi wa SNSA. Idara ya siri ya usalama wa ndani wa nchi. Nadhani umewahi kuisikia idara hiyo” alisema Julius na kunyamaza akamtazama Gavana.

“Nimekuleta mahali hapa ili mimi nawe tuzungumze”alisema Julius.

“Tu. . t. . tuzungume nini? Mmeniteka,mmenitesa,mmemtesa mke wangu,mmeua

dereva wangu na mlinzi. Nini tena cha kuzunguma nanyi? Sina cha kuzungumza nanyi. Ninachosubiri ni hatima yangu. Kama mtaniua niko tayari" alisema Gavana.

"Gavana hakuna atakayekuua japo mpango ulikuwa huo lakini nimekuondoa mahali pale nataka nikufikishe sehemu ambako utakuwa salama" alisema Julius na kuzidi kumshangaza Gavana.

"Gavana natamani kukueleza mambo mengi ili

unielewe lakini muda ni mdogo sana.” Julius alinyamaza akatazama chini kwa sekunde kadhaa halafu akamtazama Gavana.

“Gavana najua huwezi kuniamini lakini ninahitaji msaada wako”

“Msaada wangu? Gavana alishangaa

“Ndiyo Gavana. Ninahitaji msaada wako.”

“Msaada upi unauhitaji kutoka kwangu?

“Nataka unisaidie nionane na Mathew Mulumbi”

Mapigo ya moyo wa Gavana yalibadilika ghafla na kuanza kwenda kwa kasi kubwa.

“Tangu ulipochukuliwa alfajiri ya leo umeteswa na kuulizwa mahali alipo Mathew Mulumbi. SNSA walihitaji kufahamu mahali alipo Mathew lakini safari hii si SNSA wanaomtafuta Mathew Mulumbi. Ni mimi Julius Mukoke. SNSA hawahusiki tena” alisema Julius.

“Sikuelewi una maanisha nini. Unadai wewe ndiye mkurugenzi wa SNSA idara ya serikali ambayo iliniteka na kunitesa ili niwaoneshe alipo Mathew Mulumbi. Unakuja tena na kuniambia kuwa wewe ndiye unayemtafuta Mathew na si SNSA. Ninashindwa kukuelewa. Alisema Gavana.

“Sikiliza Gavana. Hadi usiku huu nilikuwa mkurugenzi wa SNSA lakini kwa sasa si mkurugenzi tena. Muda mfupi kabla sijafika kukuchukua, ilitumwa timu ya watu kuja kuniua kwa siri. Kwa

bahati nzuri niliwahi kujulishwa na mtu ambaye hakufurahishwa na maamuzi yale ya kutaka kuniua. Kama ningechelewa kwa dakika chache kuondoka nisingekuwa ninazungumza nawe hapa sasa hivi kwani ningekwisha uawa."

"Nani wanataka kukuua? Gavana aliuliza.

"Government"

"Serikali kwa nini watake kukuua?

"Gavana ndiyo maana nikakwambia inahitaji maelezo

marefu ili unielewe lakini siwezi kukudanganya. Hivi sasa ninatafutwa niuawe. That's the order from President himself. Siwezi kuukimbia mkono wa Rais. Majeshi,vyombo vyote vya ulinzi na usalama viko chini yake hivyo kunipata ni rahisi. Nimeshauriwa na watu wanaonipenda nikimbie nchini lakini baada ya kutafakari nimeona siwezi kukimbia nchi yangu. Nitapambana. Hata kama nikiuawa lakini nife nikipambana"

"Dah ! Gavana aliguna.

“Gavana ninakwambia ukweli mtupu. Hapa nilipo nafahamu mimi ni mfu mtarajiwa. Najua nitakufa lakini kabla sijafa lazima na mimi nipambane”

“Unawezaje kupambana na Rais ambaye majeshi yote yako chini yake? Aliuliza Gavana.

“Siwezi kupambana naye kwa risasi lakini ninafahmu mambo yao yote maovu na mengine nimeshiriki kuyafanya. Ninakifahamu kile ambacho Mathew Mulumbi na

wenzake wanapambana kukizuia hivi sasa. Nataka nishirikianae naye kuhakikisha mipango hiyo haifanikiwi. Hilo likifanikiwa naamini nitakuwa nimeshinda vita hii. Ninaomba tafadhali unikutanishe na Mathew Mulumbi usiku huu" aliomba Julius.

"It's hard to believe you. Kwa mambo mliyonifanyia leo, kwa udhalilishaji mkubwa mlionifanyia leo siwezi kukuamini hata kidogo. Najua hii ni moja ya njama zenu ili muweze kumpata Mathew Mulumbi. Baada ya kumpata

mtamuua pamoja na sisi sote ili kuhakikisha mipango yenu yote inafanikiwa. Niko tayari kufa kuliko kuwakutanisha na Mathew Mulumbi." Alisema Gavana.

"Gavana, huu si mtego wala si mpango wa SNSA. This is me Julius. Nahitaji sana kuonana na Mathew Mulumbi."

"Hata ungekuwa nani hutaonana na Mathew Mulumbi. Mathew ni mzalendo wa kweli kwa nchi hii na Amejitoa mhanga

kuhakikisha mabeberu na vibaraka wake hawafanikiwi mipango yao miovu dhidi ya Tanzania. Hamtamuona Mathew na ninakuhakikishia lazima wewe na wenzako wote mtajutia maovu yote mliyoyafanya kwa nchi hii.” Alisema Gavana sauti yake ikiwa kali kidogo.

“Gavana kwa nini inakuwa vigumu kuniamini? Sikiliza mzee wangu. Ninasisitiza kutaka kuonana na Mathew nina sababu nzito. Kuna kitu kinaendelea hapa nchini hivi sasa ambacho akina Mathew

wanajitahidi kuzuia kisifanikiwe. Mpango wenyewe ni kuvuruga uchaguzi mkuu ili kukiondoa madarakani chama kinachotawala sasa na kukiweka chama kingine cha upinzani. Mpango huo ni kweli upo na utafanikiwa. Nimeshiriki katika mpango huo ndiyo maana ninakwambia lazima utafanikiwa. Ni mpango ulioandaliwa kwa umakini mkubwa. Ninafahamu A-Z ya mpango huo. Nataka niwaeleze akina Mathew namna gani wanaweza kufanya kuzuia

mpango huo. Gavana mpango huu ninaokwambia ni halisi na unakwenda kutekelezwa. Usiponikutanisha na Mathew Mulumbi usiku huu,it's going to happen. Ni mpango mkubwa ambao Mathew Mulumbi na wenzake wachache hawataweza. Jambo hili ni kubwa zaidi ya uwezo wao. Wanahitaji kulifahamu kwa kina na namna gani wanaweza kulimaliza. Wasipopata taarifa sahihi kuhusu jambo hili wanaweza wakapotea. Naomba Gavana

unikutanishe na Mathew.” Alisisitiza Julius.

“Unayazungumza haya kwa sababu wenzako wamekugeuka na wanataka kukuua. Nakuhakikishia sintathubutu uonane na Mathew Mulumbi.” Alisema Gavana.

“Gavana ninakuomba mzee wangu tafadhali nikutanishe na Mathew Mulumbi. Nataka niwasaidie katika mpango wao kuhakikisha mipango ya

hujuma katika uchaguzi mkuu haifanikiwi” alisema Julius.

“Nomba usipoteze muda wako Julius. Kama una mpango wa kuniua fanya hivyo tafadhali lakini sintakukutanisha na Mathew Mulumbi” Gavana aliendelea kusimamia msimamo wake.

Julius alifikiri kidogo akauliza.

“Umeweka wapelelezi kadhaa kwa ajili ya kuutafuta ukweli kuhusu mwanao. Kuna yeyote ambaye amewahi kukupa taarifa ya kweli kuhusu

mwanao Kelvin? Aliuliza Julius. Gavana ambaye alikuwa anatazama nje alishituka akageuka na kumtazama Julius.

“Umesema nini? Aliuliza.

“Nimekuuliza kuna mpelelezi yoyote katika wale uliowaweka wachunguze kuhusu tukio la mwanao kutoweka aliyekuja na taarifa ya kweli kuhusu Kelvin?. Gavana midomo ilimtetemeka.

“Nini unakifahamu kuhusu Kelvin? Aliuliza Gavana.

“Kila kitu kuhusu Kelvin. Unafahamu kama alikuwa ni mfanyakazi wa siri wa SNSA? Aliuliza Julius.

“Hilo ninalifahamu tayari”

“Vizuri. Kama unalifahamu hilo basi ninaufahamu ukweli wote kuhusu mwanao.” Alisema Julius.

“Julius tafadhali naomba usicheze na akili yangu” alisema Mathew.

“Gavana kwa nini tusifanye makubaliano?

Nisaidie nikutane na Mathew Mulumbi na mimi nitakueleza kila kitu kuhusu mwanao Kelvin. Gavana huu si utani ninakwambia kitu cha kweli kabisa”

“Kijana narudia tena naomba usijariku kucheza na akili yangu” alisema Gavana.

“Sichezi na akili yako Gavana. Naamini ukweli kuhusu mwanao ndicho kitu kikubwa unachohitaki kujisikia kwa sasa. Nikutanishe na Mathew Mulumbi nitakueleza kila kitu” alisema Julius.

Gavana aliinamisha kichwa akafikiri kwa muda halafu akainua kichwa akamtazama Julius.

“Give me your gun” alisema Gavana. Julius bila woga alimpa Gavana bastola yake.

“Kabla sijakupeleka kwa Mathew Mulumbi,lazima kwanza nikupekue nihakikishe hauna kifaa chochote mwilini mwako” alisema Gavana. Julius hakuogopa alitoa mavazi yake akabaki mtupu. Gavana alimkagua lakini

hakukuta kifaa chochote mwilini. Gavana alikusanya mavazi ya Julius akayapekua akaikuta simu ya Julius,simu yake pamoja na pochi. Simu ya Julius haikuwa na betri. Tayari alikwisha itoa kuhofia kufuatiliwa. Aliifungua pochi ya Julius akaikagua. Alikuta kuna fedha na vitambulisho.

“Unatakiwa kuviharibu vitambulisho hivi pia” alisema Gavana.

“Hivyo vitambulisho havina tatizo lolote na

vinaweza kusaidia wakati Fulani” alisema Julius.

“Nasema viharibu vitambulisho hivi”

“Mzee vitambulisho hivyo haviwezi kutumiwa na watu wanaonitafauta. Usihofu” alisema Julius. Gavana alirejesha kila kitu katika ile pochi halafu akazikusanya zile nguo za Julius na kumtaka ashushe kioo cha upande wake.

“Unataka kufanya nini? Aliuliza Julius.

“Open the window.” Alisema Gavana. Julius alishusha kioo . Gavana alizitupa nje zile nguo.

“Umefanya nini? Aliuliza Julius.

“Unataka kuonana na Mathew Mulumbi,utafuata masharti yangu” alisema Gavana halafu akaichukua simu yake akaiwasha. Uliingia ujumbe mwingi katika simu yake hakujali. Aliitafuta namba ile ambayo Mathew aliitumia kumpigia. Aliipata akapiga simu ikaanza kuita.

****

Simu ya Israel Maungwana mwenyekiti wa chama cha ukombozi wa Afrika iliita akaipokea.

“Kudo kazi imekamilika? Aliuliza Israel.

“Mkuu,kuna tatizo limetokea. Tumefika kwa wakati mahali ulipotuelekeza lakini mlengwa tumemkosa. Tumeambiwa alikuwa hapa muda si mrefu lakini ametoweka bila kumuaga mtu

yeyote. Tumepekua kila mahali hajapatikana. Mkuu,kwa maelezo tuliyoyapata kutoka kwa watu wake tuliowakuta mahali hapo inaonekana wazi yule jamaa alifahamu kuwa tunakwenda mahali pale akatoweka kimya kimya." alisema Kudo,kiongozi wa timu ya watu sita waliotumwa kwenda kumuua Julius Mukoke.

"Sawa Kudo. Ondokeni mahali hapo na mkae katika utayari hadi hapo nitakapowapa taarifa

nyingine” alisema Israel na kukata simu.

Israel hakupoteza muda akampigia Dkt Nehemia

“Israel.” Alisema Dr Nehemia.

“Mheshimiwa Rais, kuna tatizo limetokea. Vijana wamefika eneo la tukio lakini mlengwa wamemkosa. Inaonekana alipata taarifa akatoweka. Kuna mtu yeyote ulimweleza kuhusu mpango ule wa kumuua Julius?

“Ndiyo. Nilimjulisha Charles Ombe”

“Huyo peke yake? Aliuliza Israel.

“Ndiyo. Niliona nimjulishe ili afahamu kile kinachoendelea. Nilidhani kama mwenyekiti ambaye anafanikisha jambo letu kubwa alipaswa kufahamu.” Alisema Dkt Nehemia.

“Ulifanya kosa kubwa mheshimiwa Rais. Ilikuwa ni misheni ndogo ya siri na hakuna aliyetakiwa kufahamu zaidi yetu. Tayari taarifa itafika

kwa wajumbe wengine na hiyo haitaleta picha nzuri hata kidogo.”

“Ninamuamini sana Charles, sikutegemea kama angeweza kuvujisha siri hii. Nini unanishauri nifanye?” aliuliza Dkt Nehemia.

“Nothing” alijibu Israel.

“Nothing? Kama Julius amekwisha fahamu kuwa anatafutwa auawe atakuwa ni mtu hatari sana. Vipi kuhusu Charles? Kama amevujisha siri kwa Julius lazima atawaeleza wajumbe wengine.”

“Tayari ninafahamu unakoelekea mheshimiwa Rais. Wazo lako ni kumuua Charles Ombe.”

“Ndiyo. Ni msaliti. Nilimpa siri kaivujisha. Hatufai. Ni bora tubaki na watu wawili waaminifu kuliko kuwa na jopo la wanafiki” alisema Dkt Nehemia.

“Hapana usifanye hivyo mheshimiwa Rais. Hili jambo linapaswa kushughulikiwa taratibu. Ninaomba uniachie hili suala la Julius nitalimaliza. Charles usimuulize chochote

kuhusu Julius. Kama ukizungumza naye yawe ni masuala ya mpango wetu.”

“Una uhakika utampata Julius?

“Ndiyo. Nitasaidiana na wale jamaa wakataokuwa SNSA kumsaka Julius na lazima atapatikana tu. Jambo hili ni dogo sana kwangu halinipi shida. Mheshimiwa Rais nitazungumza nawe tena kesho” alisema Israel na kukata simu.

NDUGU MSOMAJIUSIKOSE SEHEMU IJAYO.... .

MWAMBA

Naitwa Mathew Mulumbi. Ni mtanzania mzalendo. Ninaipenda mno nchi yangu Tanzania. Mimi ni mfanyabiashara. Ninamiliki viwanda kadhaa hapa nchini. Ninamiliki pia biashara nyingine kubwa. Nina hadhi ya kuitwa bilionea lakini sipendi kuitwa hivyo. Ninaamini utajiri nilio nao nimepewa na Mungu ili niwasaidie na wengine. Biashara zangu zimeajiri mamia ya watu na hilo ni jambo jema sana

ambalo hunifanya niwe na furaha kila siku.

Kabla ya kuingia katika biashara,nilifanya kazi katika shirika la ujasusi Tanzania. Japokuwa kwa sasa si mfanyakjazi wa shirika hilo lakini nimekuwa nikishiriki katika misheni mbali mbali muhimu kwa usalama wa nchi. Wakati mwingine nimekuwa nikiombwa na serikali kushiriki katika misheni hizo hasa kutokana na uzoefu wangu. Wakati mwingine nimekuwa nikishiriki katika misheni mbali mbali kimya

kimya nikishirikiana na washirika wangu wa karibu,Papi Gosu Gosu,Ruby,Agai na wengineo.

Ninapokusimulia mkasa huu mpenzi msomaji, niko katika mtafaruku mkubwa sana na bilionea mkubwa nchini Tanzania aitwaye Amos Igunga. Ni mtu mwenye nguvu. Mtafaruku wetu umepelekea nianze kuvuta harufu ya umasikini. Baadhi ya biashara zangu zimefungwa. Nimefunguliwa kesi mbaya ya uhujumu uchumi nikidaiwa kukwepa kodi. Muelekeo wa

kesi si mzuri,hofu ya kufilisiwa ni kubwa.

Chanzo cha mgogoro huu ni mhandisi Omega Benson. Huyu ana mahusiano ya kimapenzi na bilionea Igunga. Mambo yote yalianza baada ya kampuni ya Omega Constructions inayomilikiwa na Mhandisi Omega Benson kupewa kazi ya kujenga moja ya kiwanda changu kipya cha kutengeneza viatu. Sitaki kuelezea sifa za Omega lakini fahamu ni mwanamke mrembo mno. Mambo yalianza taratibu kwa urafiki

wa kawaida lakini baadaye tulijikuta katika penzi zito. Taarifa zilimfikia bilionea Igunga na alimtaka mpenzi wake huyo kuachana haraka sana na mimi. Kitendo hicho kilipelekea penzi la Omega na bilionea kuvunjika na rasmi ilianza vita kati yangu na bilionea Igunga.

Mpambano wetu umepelekea nigundue mambo mengine makubwa na mazito kuhusiana na bilionea huyo. Japo kesi inaendelea mahakamani lakini nimelazimika kuingia katika

misheni nzito. Nimeapa kupambana na bilionea huyu kwa kila hali. Licha ya nguvu alizo nazo,nataka nimuoneshe kuwa mimi ni MWAMBA.

USIKOSE RIWAYA HII YENYE MSISIMKO WA AINA YAKE 2021

DEAR MATHEW MULUMBI.

Ritha Mwikala aligundua mumewe hakuwa sawa. Alihisi kuna kitu kilichokuwa kinamtatiza akilini. Baada ya chakula cha usiku,Rais Solomon Mwikala hakujumuika na familia yake kwa maongezi kama ilivyo kawaida yake,aliinuka na kuelekea chumbani kwake. Mke wake alimfuata na kumsemesha kwa sauti ya upole akitaka kufahamu kile kinachomsumbua mume wake.

“Ninatakiwa kuweka saini yangu ili Mathew Mulumbi anyongwe” alisema Rais Solomon. Mke wake alimtazama kwa makini halafu akauliza.

“Kwani kuna ugumu gani kusaini kunyongwa kwa huyo mtu?

“Ugumu uliopo ni kwamba zimepita awamu mbali mbali za uongozi na maraisi wote hawajanyonga watu. Mimi hata kipindi cha kwanza sijamaliza ninatakiwa kusaini

ili Mathew Mulumbi anyongwe.”

“Sioni tatizo. Kama sheria inakutaka ufanye hivyo,hakuna tatizo. Saini” alisema Ritha.

“Ninasita. Mathew Mulumbi pamoja na yote aliyofanya lakini ni shujaa wa nchi hii. Ingekuwa ni kwa ridhaa yangu nisingekubali lakini ninapata shinikizo kubwa la kutekeleza adhabu hiyo ya kifo. Mbaya zaidi wanaoshinikiza ni wale

waliofanikisha sisi kuwepo hapa.”

“Solomon huna cha kuhofia. Just sign” alisema Ritha.

USIKOSE SIMULIZI HII MAPEMA 2021.